*Mwongozo wa Utafiti wa Kibiblia*

# Miguuni Pake Yesu



## Ngazi ya 3

Miguuni Pake Yesu

# Kielezo cha Mada ya Mwongozo wa Utafiti wa Kibiblia

## Ngazi ya I

- ❑ 1 Tajiri Asiyejitambua
- ❑ 2 Je, Yawezekana Kuufahamu Wakati Ujao?
- ❑ 3 Chanzo cha Maumivu Mengi ni Nini?
- ❑ 4 Hatua Nne Kuelekea kwenye Amani ya Ndani na Furaha
- ❑ 5 Namna ya Kuboresha Utu Wetu
- ❑ 6 Ufumbuzi Bora Zaidi kwenye Matatizo na Yanayonihusu
- ❑ 7 Je, Ni Nani Atakayeitawala Dunia Hatimaye?
- ❑ 8 Sababu za Mashaka ya Dunia Yaliyopo
- ❑ 9 Tukio Kubwa Zaidi la Milenia ya Tatu

## Ngazi ya 2

- ❑ 10 Siri ya lile Sanduku la Dhahabu la Agano
- ❑ 11 Mfumo wa Maisha Unaoleta Usalama na Amani
- ❑ 12 Kumi Kutoa Moja ni Sifuri
- ❑ 12a Kioo na Kivuli
- ❑ 13 Njia Bora Zaidi ya Kuushinda Msongo
- ❑ 14 Udanganyifu Mbaya Zaidi katika Historia
- ❑ 15 Viwango Viwili vya Upendo
- ❑ 16 Je, Kuna Maisha baada Kifo?
- ❑ 17 Ushauri wa Kimbingu dhidi ya Nguvu Zisizoelezeka
- ❑ 18 Kitabu cha Ufunuo na Hatima ya Sayari Yetu
- ❑ 19 Maono Juu ya Ulimwengu Ulio Bora Zaidi

## Ngazi ya 3

- ❑ 20 Je, Mpinga Kristo Yupo Tayari?
- ❑ 21 Unabii wa Kushangaza wa Miaka 2,300
- ❑ 22 Utetezi Wangu Mbele ya ile Mahakama Kuu
- ❑ 23 Je, ni Kwa Nini Kumekuwako na Dini Nyingi Sana?
- ❑ 24 666 na Marekani Katika Unabii
- ❑ 25 Siku ya Muhimu Zaidi Katika Maisha ya Mtu
- ❑ 26 Namna ya Kumtambua Nabii wa Kweli
- ❑ 27 Funguo Saba Kwenye Maisha ya Kiafya
- ❑ 28 Namna ya Kutatua Matatizo Yangu ya Kifedha
- ❑ 29 Uzuri Halisi
- ❑ 30 Siri ya Mafanikio



# 20 JE, MPINGA KRISTO YUPO TAYARI?



Lau kama kuna nadharia nyingi juu ya mpinga Kristo, kuna ufunuo mmoja pekee unaostahili kutumainiwa-Unabii wa Biblia. Neno hili mpinga Kristo linamaanisha nini? Mpinga = kinyume na Kristo. Anapinga vyote, mafundisho ya Yesu Kristo na anampinga Yesu Kristo Mwenyewe. Kujifunza mada hii kunaweza kusababisha mshangao, huzuni, hasira, kukatishwa tamaa ama kuridhishwa. Danieli nabii alifadhaika sana pale alipoupokea ufunuo huu (Danieli 7:15, 28). Mungu ametupatia sisi unabii ili kwamba tuwe nayo nuru na kuifahamu ile kweli (2 Petro 1:19).

## MPINGA KRISTO

**1. Je, wapinga Kristo walikuwako hata katika wakati wa mitume? 1 Yohana 2:18, 19; Wagalatia 1:6, 7.**

*Walikuwa ni ndugu, kwa sababu anasema: "Walitoka ________________________________ ."*

**2. Je, huyu mpinga Kristo ni mamlaka fulani isiyomkiri Mungu, ama ilidai kuwa ni ya Kikristo? Tito 1:16.**

*Wanakiri ya kwamba ____________________ Mungu; bali ______________________________*

a) Wanajihesabia wao wenyewe sifa zinazomhusu Mungu pekee; utakatifu, kutoweza kukosea, kutoweza kubadilika (2 Wathesalonike 2:3, 4).

b) Anawapinga na kuwatesa wanafunzi wa Kristo (Ufunuo 13:7).
   - Mbinu aliyoitumia Kristo ni upendo-sio maogofyo, kutiwa maumivu makali, kutiwa hofu, ama mateso.

c) Anaishambulia sheria ya Mungu na kusimamisha sheria za kibinadamu pamoja na mapokeo (Mathayo 15:8, 9).
   - Kinyume chake, Kristo aliziimarisha, akafundisha, na kuzishika zile amri. (Yohana 15:10).

d) Mpinga Kristo anahubiri wokovu kwa matendo ya kibinadamu (2 Wathesalonike 2:10).
   - Kristo anaonesha ya kwamba wokovu ni kwa njia ya imani na matendo yetu ni matunda ya upendo wa Kristo unaofanya kazi ndani yetu. Huyu mpinga Kristo katika unabii ni nani? Kitabu cha Danieli, ambacho kiliandikwa yapata zaidi ya miaka 2,600 iliyopita, kinaifunua siri hii.

## FUNGUO SABA ZA UNABII

**3. Je, pepo na maji humaanisha nini katika unabii?**

- *Pepo huwakilisha vita (Yeremia 49:36, 37).*
- *Maji huwakilisha ____________________________________________(Ufunuo 17:15).*

**4. Je, wanyama, vichwa, mabawa na pembe huwakilisha nini?**

*Wanyama huwakilisha falme (Danieli 7:23). Vichwa na pembe huwakilisha mpasuko katika falme hizo (Danieli 7:24). Mabawa huwakilisha kasi (Habakuki 1:8). Mataifa mengi leo bado yanawakilishwa na mifano kama hii: Marekani inawakilishwa na tai; Uingereza inawakilishwa na simba; Urusi inawakilishwa na dubu; China inawakilishwa na joka; Ufaransa inawakilishwa na jogoo. Katika unabii, siku moja ni sawa na mwaka mmoja (Ezekieli 4:6; Hesabu 14:34).*




## *MATAIFA MANNE KATIKA UNABII*

**6. Danieli aliona nini katika maono? Danieli 7:2, 3.**

- ____________________________ nne zilivuma juu ya __________________________________, ikimaanisha ya kwamba kungekuwako na vita miongoni mwa watu hawa wengi.
- ___________________________________ wanne walitokea baharini.

**7. Wale wanyama wanne wanawakilisha nini? Danieli 7:16, 17, 23.**

_________________________________________________________________________________

- *Hawa ni falme zile zile zinazowakilishwa katika ile sanamu ya Danieli sura ya 2.*

**8. Mnyama yule wa kwanza alikuwa na tabia gani? Danieli 7:4.**

________________________________ *mwenye* ___________________________________ *mawili.*

a) Anawakilisha Babeli (606-538 K.K.).

b) Kama vile dhahabu ilivyo kito chenye thamani zaidi, simba ni mfalme wa pori.

c) Mabawa mawili yanawakilisha ushindi wa kasi wa Nebukadneza.

**9. Mnyama wa pili alionekanaje? Danieli 7:5. __________________________________________**

a) Anawakilisha Umedi na Uajemi (538-331 K.K.).

b) Aliegama upande mmoja, ikiwakilisha ubora wa Waajemi juu ya Wamedi.

c) Alikuwa na mbavu tatu kinywani mwake, ikionesha ushindi wake katika majimbo matatu-Babeli, Lidia, na Misri.

d) Alikula nyama nyingi, kumaanisha kwamba walikuwa wakali sana katika kupata ushindi wao.

**10. Je, ni tabia gani katika chui huyu inayotajwa katika mstari wa 6?**

*Alikuwa na ____________________________ na ______________________________. Hii inawakilisha Utawala wa Uyunani (331-168 K.K.).*

a) Mabawa manne yanawakilisha kasi ya ushindi wao-mara mbili zaidi ya ule wa Nebukadneza. Ilimchukua Alexanda Mkuu miaka 8 pekee kuweza kuiteka nchi ipatayo kilometa za mraba milioni 5.

b) Vichwa vinne: wakati Alexanda Mkuu alipokufa (323 K.K), ufalme wake uligawanywa miongoni mwa majenerali wake wanne: Linsimakus akatawala katika Thrace; Kasanda akatawala katika Uyunani; Selekus akatawala katika Siria na Babeli, naye Ptolomi akatawala katika Misri.

**11. Mnyama wa nne alikuwa kama nini? Mstari 7, 19, 20, 23.**

______________________________________________________________________

a) Mnyama wa nne anawakilisha Rumi (169 K.K.-176 B.K.). Ukatili wake unawakilishwa na yale makucha ya shaba na meno ya chuma.

b) Zile pembe kumi zinalingana na vile vidole kumi katika Danieli 2, navyo huwakilisha mataifa kumi ya Ulaya Magharibi, ambayo yalikuwapo katika wakati wa kumalizika kwa Utawala wa Rumi (mstari 24).

## *ILE PEMBE NDOGO*

**12. Je, pembe ile iliyozuka ilionekaneje? Mstari 8, 20-25.**

*Pale pembe hii ilipozuka,* ______________________________________ *ziling'olewa. Ilikuwa na* ____________________ *kama wa mwanadamu na* ________________ *kilichonena mambo makuu.*

a) Ilikuwa ni tofauti na zile pembe nyingine, jambo ambalo linamaanisha ya kwamba haikuwa ni mamlaka ya kisiasa bali ni mamlaka ya kidini. Je, ni mamlaka gani ambayo ilijitwalia nafasi mahali pa Rumi ya Kifalme? Ni Upapa.

b) Huyu alikuwa mkubwa kuliko wale wanyama wengine, kando ya ile mamlaka yake ya kidini alikuwa pia na mamlaka ya kisiasa. Mvuto wake bado una nguvu hata leo.

c) Zile pembe tatu ambazo ziling'oka pale pembe hii ilipozuka inawakilisha wafalme watatu ambao walipigwa na kuangamizwa kabla ya kuanzishwa kwa upapa. Panapo mwaka 493, Waheruli walipigwa; mwaka 534, Wavandali waliangamizwa; na mnamo 538, Waostrogothi waliangamizwa na Wajastinia.

d) Ingesema maneno kinyume Chake Aliye Juu. Papa anajiita mwenyewe kuwa asiyeweza kuanguka, anatoa vyeti vya msamaha, na anajiita mwenyewe kuwa ni Baba Mtakatifu, sifa ambazo zinamhusu Mungu pekee (Mathayo 23:9).

**13. Je, ile pembe ndogo ingewafanyeje wale watakatifu, waumini halisi? Danieli 7:21.**

______________________________________________________________________

*Jambo hili linatukumbusha sisi juu ya zama za giza zilizotajwa katika historia, wakati ambapo mamilioni ya Wakristo ambao waliitwa kuwa ni wazushi, waliuawa kwa njia mbali mbali za kutisha katika kile kipindi cha "Baraza la Kuu la kuwahukumu wazushi wakidini."*



**14. Je, mamlaka ile ilifikiri kubadilisha nini kwa kulingana na unabii huu? Mstari 25.**

__________________________________________________

*Zile Amri Kumi zilibadilishwa. Katika katekisimo, amri ya pili imerukwa na ile amri ya kumi imegawanywa kuwa mbili. Amri ya nne, ambayo inaagiza utunzaji wa Sabato (Jumamosi) imebadiliwa na "ishike kitakatifu siku ya Bwana." Mungu hajamwidhinisha mtu ye yote kuibadilisha sheria Yake takatifu (Mathayo 5:16, 17; Muhubiri 3:14).*



**15. Je, yale mateso yangedumu hata lini? Danieli 7:25, sehemu ya mwisho.**

________________________________________________________

*Wakati ni sawa na mwaka, na nyakati mbili ni sawa na miaka miwili; na nusu ya wakati ni sawa na nusu ya mwaka, ikijumlishwa ni miaka mitatu na nusu. Tunauhesabu mwaka wa kibiblia kuwa na siku 360, ni siku 1,260. Hesabu hii kama ile iliyotajwa katika Ufunuo 12:6, 14 na 13:5. Siku hizi 1,260 za kinabii ni sawa na miaka halisi 1,260. Hiki ni kipindi kinachoanzia mnamo mwaka 538, pale upapa ulipoanza kutawala, hadi mwaka 1798. Katika kile kipindi cha Mapinduzi ya Ufaransa, Napolioni alimtuma Jenerali Berther akamkamate Papa Pius VI mateka. Papa huyu alifia kule uhamishoni.*

## *HITIMISHO*

- Mungu Mwenyewe ndiye anayeongoza hatima ya mataifa.
- Unabii unaeleza juu ya maendeleo ya historia na ile vita kati ya nuru na giza, lakini Kristo Ndiye mshindi, na wale wote wanaomwamini watashiriki katika ule ushindi mkubwa.
- Unabii unaonesha ya kwamba Kristo hataibadili ile sheria Yake, bali yule mpinga Kristo anajaribu kufanya hivyo. Wala wanadamu wasiibadili kweli ya Mungu.
- Hebu na tutambue ya kwamba uthabiti wa milele wa zile Amri Kumi kwa sababu Yesu Kristo anatutaka tuzitunze na anataka kuwabariki wale wanaompokea Yeye kama Mwokozi na Bwana wao.

---

***Uamuzi wangu:*** *Ninatambua ya kwamba Kristo hakuibadili ile Sheria Takatifu ila hii ni kazi ya mpinga Kristo.* ❑ *Ndio* ❑ *Hapana*

---

# 21 UNABII WA KUSHANGAZA WA MIAKA 2,300



Kuna nabii za kushangaza zipatazo 2,300 katika Biblia. Hizi zina usahihi wa matabirio ya kimahesabu sahihi zaidi ya kumi. Hizi zimekuwa ni kama uso wa saa ya Mungu. Katika unabii wa miaka 2,300, mafunuo yenye kushangaza yanatuonesha sisi juu ya maendeleo ya historia-kuinuka na kuanguka kwa falme mbali mbali, mwaka wa kubatizwa kwa Kristo na ule wa kufa Kwake, wakati ambapo ile kweli ambayo yule mpinga Kristo aliyoiangusha itakaporejeshwa, pamoja na mwanzo wa ule wakati wa mwisho. Ni unabii unaopasa kufahamiwa!

## *UNABII WA DANIELI 8*

**1. Je, Danieli aliona nini katika maono alipokuwa katika kingo za mto Ulai? Danieli 8:3-9.**

- ______________________ mwenye pembe mbili, moja ilikuwa _______________ kuliko ile nyingine, na kondoo mume huyu alisukuma kuelekea kaskazini na kusini, akiwajeruhi wapinzani wake. Hapana mnyama yo yote angeweza kumzuwia.
- ________________________ alitokea upande wa magharibi, kwa kasi kabisa kiasi kwamba hakugusa nchi. Alikuwa na _____________________________ kati ya macho yake. Akamrusha ____________________ na kuzivunja pembe zake mbili. Kisha, ilipokuwa na nguvu zaidi, ile pembe yake yenyewe ilivunjika na pembe nne zilizuka mahali pake.
- Kutoka katika mojawapo kulitokea _________________________, iliyokua sana kuelekea kusini, mashariki na upande wa ___________________________ (Palestina).


**2. Kondoo mume aliwakilisha nani? Mstari 15, 16, 20.**

*Aliwakilisha _____________________________.*

*Alizielekeza pembe zake kuelekea mashariki (Uyunani), kaskazini na kusini (Misri). Unabii huu ulitimilika mnamo 550 K.K. wakati Babeli ilikuwa bado inatawala.*


**3. Huyu beberu aliashiria nini? Mstari 21, 22.** ______________________________________

*Mfalme wake wa kwanza alikuwa ni Alexanda Mkuu. Maelezo haya yasemayo "bila kuigusa nchi" yanaonesha kasi ya Alexanda katika ushindi. Katika miaka 8 pekee aliweza kuiteka dunia yote iliyofahamika katika zama zile, na utawala wake ulifika mbali hata India. Alikufa katika upeo wa utukufu wake. Pembe nne-majenerali wanne walimrithi Alexanda, nao wakaugawa ufalme huo katika sehemu 4: Makedonia, Thrase, Siria-Babuloni na Misri.*






# UNABII WA KUSHANGAZA WA MIAKA 2,300




ESCALA PROFÉTICA: 1 DÍA = 1 AÑO (Números 14:34; Ezequiel 4:6)

**4. Kulitokea nini katika moja ya pembe zake? Mstari 9, 23, 25.**



*Hebu linganisa mistari hii na ile pembe ndogo ya Danieli 7. Pembe ile iliyokua inaelekeza kwa Rumi katika pande zake mbili: Rumi ya kipagani na Rumi ya kipapa. Ilikua, na ushindi wake ulipanuka kuelekea mashariki kufikia Uyunani, Asia, na kuelekea kusini kufikia Afrika, Karthage na Misri. Ile nchi ya uzuri hapa inahusu Palestina. "Na mahali pa patakatifu pake pakaangushwa chini," (mstari 11). Rumi ilimpinga Kristo. Mnamo 70 B.K., jeshi la Rumi liliiangamiza Yerusalemu. Rumi ya kipapa ilikuwa ni mwendelezo wa ile Rumi ya kipagani ya wale Makaisari nayo ingeweza "kuwaangamiza …… watu watakatifu," (mstari 24). Hii inaelekeza kwenye lile Baraza la Kikanisa la Kuwahoji Wazushi wa kidini (Inquisition). "… ikamwondolea sadaka ya kuteketezwa ya daima" (mstari 11). Tunahesabiwa haki na Kristo; Yeye Ndiye anayetuombea sisi. Lakini kanisa likaunda safu za waombezi wa kibinadamu. Kwa njia ya kuanzishwa kwa misa, ambamo ndani yake kasisi anakuwa ndiye mwombezi, ndipo lile fundisho la kuhesabiwa haki kwa njia ya matendo, likamwondoa Kristo. Iliitupa chini ile kweli, ikitenda vile ionavyo yenyewe na kustawi. Ilithubutu kuibadili ile sheria ya Mungu kwa kuweka Jumapili mahali pa Sabato ya Biblia na kuanzisha amri za kibinadamu.*

**5. Swali linakuja: "Na lile kosa lifanyalo ukiwa, yataendelea hata lini?" (Mstari 13).**

*Kwa maneno mengine ni, hata lini ambapo huyu mpinga Kristo ataificha kweli juu ya uombezi unaoendelea wa Kristo kwa ajili ya wenye dhambi? Ni kwa muda gani ambapo watu wa Mungu wataendelea kuteswa? Hata lini hii kweli itaendelea kutupwa chini na sheria ya Mungu kukanyagwa mavumbini? Je, hukumu hii itaahirishwa hata lini? Jibu lake lilikuwaje? (Mstari 14).*

**6. Siku hizi 2,300 zilikihusu kipindi gani cha wakati? Mstari 17, 19, 26.**

*Juu ya wakati wa ____________. Danieli hakuweza kuyaelewa maono haya ya siku 2,300; ikamtia hofu sana hata akaugua. Mstari 26, 27.*

## *MAFUNUO YANAYOUFUNGUA UNABII WA DANIELI 9*

Baada ya sala ya juhudi ambamo ndani yake Danieli alijinyenyekeza mwenyewe kwa Mungu, akapokea jibu (Danieli 9:20-23), akapokea maelezo kamili juu ya miaka 2,300 iliyotajwa katika sura iliyotangulia.

**7. Je, ni majuma mangapi ya kinabii yaliyokusudiwa ama kukatwa kutoka katika zile siku 2,300 kwa ajili ya watu wa Israeli? (Mstari 24).**

*Je, kuna miaka mingapi halisi katika yale majuma 70 ya kinabii? Tukitumia ufunguo wa kinabii wa siku 1 = mwaka 1 (Ezekieli 4:6; Hesabu 14:34), tunapata kwamba majuma 70 zidisha kwa siku 7 za juma = 490 siku za kinabii ama miaka 490 halisi.*

**8. Je, kungetokea nini katika miaka hii 490 ya rehema kwa Wayahudi? Mstari 24.**

*____________ ingeishilizwa, na ___________________ ungefikiwa kwa njia ya kafara ya Kristo. Maono pamoja na unabii ungetiwa muhuri, kadiri ya nabii zile 333 kumhusu Yesu zilitimilika. Mtakatifu wa watakatifu ange____________________. Jina hili Kristo linamaanisha "mtiwa mafuta".*

**9. Mwanzo wa miaka 2,300 na yale majuma 70 yaliyo sehemu ya unabii huu ni nini? Danieli 9:25.**

*Tarehe ile ambapo agizo la ______________________________________________________.*

*Mwanzo wa mahesabu haya ni katika mwaka 457 K.K. (katika robo ya tatu), pale ambapo Artashasta, mfalme wa Uajemi, alipotia saini tamko la kuujenga upya mji wa Yerusalemu, (Ezra 7:7; 6:14). Yerusalemu uliachwa kwa sababu Wayahudi walipelekwa uhamishoni kule Babeli.*

**10. Je, ni katika mwaka gani ambapo zile siku 2,300 zingeisha?**

*Kuna miaka 456 na robo moja katika zama zile za K.K. ili kukamilisha miaka 2,300, tunahitaji miaka 1,843 na robo, na hii hutuleta kwenye robo ya tatu ya mwaka 1844 B.K, ambayo ni miaka 2,300 kamili. Mwaka 1844 ndio mwisho wa kipindi hiki kirefu cha kinabii.*

## *UNABII WA MAJUMA 70*

**11. Je, kungekuwa na majuma mangapi kufikia kuja kwa Masihi? Danieli 9:25.**

*Majuma ________________________ na majuma ____________________________________ .*

a) Majuma saba ni siku 49. Huu ulikuwa ndio wakati uliotumika katika kulijenga hekalu pamoja na kuta za Yerusalemu. Miaka hii inatufikisha wapi? Mwaka 408 K.K. (407 na robo).

b) Kuufikia mwaka wa kubatizwa Kwake Kristo, tunahesabu majuma 62 x 7 = miaka halisi 434. Tunatoa miaka hii kutoka kwenye mchoro wetu tulianzia na mwaka 407 na robo, na tunabakiwa na miaka 26 na robo tatu. Hii inatuleta sisi kwenye mwaka 27 B.K., mwaka ambao Kristo alibatizwa. Wagalatia 4:4; Mathayo 3:13-17.

**12. Ni katika mwaka gani ambapo Kristo angesulibiwa? Danieli 9:26, 27.**

*Baada ya majuma sitini na miwili: Ili kuyakamilisha yale majuma 70, tunahitaji juma moja (miaka 7). Je, kungetokea nini katika juma hili la mwisho ama miaka saba? Yale majuma 62 yaliishia katika mwaka 27 B.K.; na tukiongeza miaka 7 tunaufikia mwaka 34 B.K.*

*Katikati ya juma, sadaka na kafara zingekomeshwa. Huu ndio mwaka 31 B.K., katika mwezi wa Nisani katika kalenda ya Kiyahudi, ambao unalingana na mwezi wetu wa Aprili, katika mkesha wa pasaka ya Kiyahudi. Yesu alisulibiwa panapo tarehe hiyo, kunako masika ya mwaka 31 B.K., kwa agizo la Pilato.*

*Unabii wa Biblia ni sahihi kabisa! Kafara hii ingeweza kukoma kwa sababu zilikuwa ni mfano wa Kristo. Pale alipokufa kwa ajili ya dhambi zetu, hapakuwa na haja tena ya kumwaga damu ya wanyama. Pale Yesu alipokufa, pazia la hekalu lilipasuka vipande viwili (Mathayo 27:51).*

**13. Je, kipindi walichopewa Israeli kama watu wa Mungu kiliisha lini? Kukatokea nini katika Yerusalemu? Mstari 24, 26.**

*Mwishoni mwa majuma ______________________ ama miaka _____________________________ .*

*Kipindi hiki kiliisha katika mwaka 34 B.K. Miaka mitatu na nusu baada ya kifo cha Yesu, injili ilihubiriwa kwa Wayahudi pekee. Askari wa Kirumi wakauzingira mji wa Yerusalemu mnamo mwaka 70 B.K., na baada ya kuutiisha mji kwa njaa, ukatwaliwa, ukachomwa moto na kuteketezwa, ukiacha wakazi wake wapatao zaidi ya milioni wakiwa wamekufa.*

## *HITIMISHO*

Usahihi wa unabii wa Biblia, hususani ukokotozi wa hesabu hizi, ni muhuri ama dhamana ya uthabiti wa kibiblia na ni uthibitisho usiokanushika ya kwamba Kristo alikuwa ndiye Masihi aliyeahidiwa. Mwishoni mwa miaka 2,300 mnamo 1844 panaonesha muda ule wa kurejeshwa kwa ile kweli na kutakaswa kwa hekalu.

Je, hili linamaanisha nini? Hili tutaliona katika mada ijayo.

---

***Uamuzi wangu:*** *Ninaamini kwamba siku 2,300 ziliisha mnamo 1844 na ya kwamba kutokea hapa kurejeshwa kwa ile kweli kulianza.* ❑ *Ndio* ❑ *Hapana*

---

# 22 UTETEZI WANGU MBELE MAHAKAMA KUU



Katika mojawapo ya mifano ya Yesu, tunasimuliwa kisa cha mfalme aliyefanya karamu ya arusi ya mwanawe. Mathayo 22:1-14.

- Mwaliko wa kuja arusini ni injili.
- Mwaliko wa kwanza walipewa watu wa Israeli tokea wakati wa ubatizo wa Yesu hadi mauti Yake.
- Mwaliko wa pili pia ulitolewa kwa Wayahudi baada ya kifo cha Kristo, kwa miaka mitatu na nusu zaidi, hata kifo cha Stefano.
- Mwaliko wa tatu, mara baada ya Wayahudi kuukataa mwaliko wa Mungu, ukaelekezwa kwa Mataifa.
- Ni wapi ambako wageni hawa, walioalikwa kutoka katika mitaa na kando ya barabara, walikopata mavazi yao ya arusi?

Katika nyakati za kale, ilikuwa ni desturi kule Mashariki kwa mfalme kutoa mavazi rasmi kwa ajili ya sherehe kwa kila mgeni anapoingia kwenye ukumbi. Vazi hili ni ishara ya haki Yake Yesu. Anayafunika matendo yetu machafu yaliyopita na kututamka sisi kama wenye haki. Mtu yule asiyevaa vazi la arusi atasimama mbele ya hukumu. Iwapo hatuvai vazi la haki ya Kristo, iwapo hatumpokei Kristo kama Mwokozi na Bwana wetu na tusiyatende mapenzi Yake, tunahukumiwa na kutupwa mbali ya uwapo wa Mungu.

## *HUKUMU YA UPELELEZI*

**1. Je, Mungu ataangalia nini katika ile hukumu? Mhubiri 12:14; 2 Wakorintho 5:10.**

_______________________________________________

*Pale Yesu Kristo ajapo kuwafufua watakatifu waliokufa wawe hai na kwenda pamoja Naye, uamuzi juu ya watakaookolewa na wale watakaopotea utakuwa ulikwisha fanyika. Hukumu ya upelelezi itakuwa ilikwisha fanyika. Je, ni lini ambapo hukumu hii itafanyika? Je, ni lini pale ambapo Mfalme atakuja kuona kama kila mmoja amevaa lile vazi la arusi? Hii ni siku makini kabisa. Matendo 17:31.*

**2. Danieli aliiona hukumu hii ya upelelezi katika maono. Je, ni nani watakaohusika? Danieli 7:9, 10, 13, 14.**

- Hakimu ni ____________________.
- Sisi tu washitakiwa
- Mashahidi ni malaika. Je, kuna malaika wangapi? (mstari 10) ________________________
- Uthibitisho ni kile kilichoandikwa katika vile vitabu (Ufu. 20:12).
- Mshitaki ni Shetani (Ufu. 12:10).
- Sheria ambayo tutahukumiwa kwayo ni ______________________ ya Mungu (Yakobo 2:12).
- Mtetezi wetu ni _____________________________ (mstari 13; 1 Yohana 2:1).

**3. Dhambi zetu zinaandikwa katika hekalu la Mungu. Hukumu ya upelelezi pamoja na huduma ya utakaso ni muhimu. Je, haya yangeanza lini, kwa kulingana na unabii wa Danieli 8:14?**

a) Zile siku ama miaka _____________________________ ilikwisha mnamo 1844, ambapo ndipo mwanzo wa hukunmu ya upelelezi.

b) Hapa ndio mwanzo wa wakati wa mwisho na kurejeshwa kwa ile kweli ambayo ilikanyagwa mavumbini na yule mpinga Kristo. Kweli hizi makini zikaanza kuhubiriwa.

c) Pia ulikuwa ni mwanzo wa kipindi cha mwisho cha kanisa la saba la Laodikia. Ulikuwa ni mwanzo wa hukumu ya upelelezi kule mbinguni-kutakaswa kwa hekalu kwa kuainisha kama ni nani watakaookolewa na nani watakaopotea, kabla ya kuja kwa Yesu. Ili kuelewa kwa wazi juu ya maana ya "kutakaswa kwa hekalu", tunapasa kuangalia katika Agano la Kale na tujifunze juu vile vivuli.

## *KUTAKASWA KWA HEKALU LA KIDUNIA*

**4. Je, Mungu aliwaagiza Waisraeli wafanye nini? Kutoka 25:8.**

____________________________________________________________

**5. Kulipaswa kumwagwa nini ili kwamba mwanadamu aweze kusamehewa? Waebrania 9:22, 12.**

____________________________________________________________

*Mungu akamwambia Adamu na Hawa, "Msiyale ….. msije mkafa." Mwanadamu akafanya dhambi naye akahukumiwa kufa, lakini Kristo akakubali kufa mahali pa mwanadamu. Hata pale wakati ulipowadia, mnyama alitolewa kafara, akiwakilisha ile kafara ya Kristo (Waebrania 9:9).*

**6. Katika lile hekalu lililojengwa mle jangwani, kulikuwa na vyumba viwili vilivyotenganishwa na pazia, Mahali Patakatifu na Patakatifu Mno. Je, ni mara ngapi makuhani waliingia Mahali Patakatifu, na ni kwa kusudi gani? Waebrania 9:6.**

____________________________________________________________

*Katika Walawi 4 tunasoma juu ya aina mbali mbali za dhambi: Iwapo mtu alitenda dhambi, alitakiwa kuleta mnyama asiye na ila, aweke mikono yake juu ya kichwa cha yule mnyama, kwa jinsi hiyo azihamisha dhambi zake kwenda kwa yule mnyama, na kisha anamwua. Ndipo, kuhani alitwaa ile damu, akainyunyiza katika pembe za ile madhabahu, na kumwaga ile iliyobaki chini ya madhabahu. Iwapo kuhani ama kusanyiko la Israeli lilitenda dhambi, alilazimika kuitwaa sehemu ya damu kutoka kwa ile kafara, na kisha aingie hata Mahali Patakatifu na kuinyunyiza ile damu katika pazia. Kwa jinsi hii, aliihamishia ile dhambi hekaluni.*

**7. Je, ni nani pekee aliyeingia Mahali Patakatifu Mno, na mara ngapi? Waebrania 9:7.**

____________________ *aliingia Mahali Patakatifu Mno mara moja kwa* ____________________ .

- Katika ile siku ya Upatanisho, hekalu lilitakaswa. Kwanza, kuhani mkuu alitoa kafara ya ng'ombe mume kwa ajili yake yeye mwenyewe pamoja na familia yake. Kisha, aliwatwaa mbuzi wawili na kupiga kura juu yao, mmoja akiashiria kwa Bwana, na mwingine, wa Shetani. Yule aliyemwakilisha Yesu alitolewa kafara. Kuhani mkuu aliitwaa ile damu na kuingia nayo hata Patakatifu Mno katika wingu la uvumba; hapo alinyunyiza katika kile kiti cha rehema, Sanduku la Agano, ambalo lilikiwakilisha kiti cha enzi cha Mungu, mara saba kwa kidole chake. Pale Mahali Patakatifu Mno palikuwa na nuru ya ile SHEKINA ama uwapo wa kimbingu. Ile sheria iliyovunjwa ilidai kifo cha yule mtenda dhambi na ya kwamba ile sheria ilikuwa chini ya kiti cha rehema. Pale kuhani aliponyunyiza ile damu, rehema ilitolewa kwa mvunjaji yule wa sheria. Jinsi hii, lile pazia lilitakaswa tu kwa uwapo wa Mungu katika mahali pale na watu walisamehewa (Walawi 16:16). Kisha walimleta yule mbuzi, naye kuhani mkuu aliweka mikono yake juu ya kichwa chake na kuziungama dhambi zote za Israeli na kisha mnyama yule alipelekwa jangwani.

## *HEKALU LA MBINGUNI*

**8. Hekalu halisi liko wapi? Waebrania 8:1, 2.**

____________________________________________________________

**9. Ni nani aliye Kuhani Mkuu katika hekalu la mbinguni? Waebrania 9:24.**

____________________________________________________________

*Hekalu la Mungu lilifunguliwa kule mbinguni (Ufu. 11:19) naye Kristo alionekana akivaa mavazi ya kuhani (Ufu. 1:12-15), naye akitembea kati ya vile vinara vya taa. Alijiwakilisha Yeye Mwenyewe, katika namna ya malaika, kama mwenye kuhudumu mbele ya ile madhabahu, akishika chetezo cha dhahabu na akipokea maombi ya watakatifu (Ufu. 8:3, 4).*

**10. Je, alitoa damu ya nani? Waebrania 9:11, 12.**

______________________________________________________________________

- Katika Ufunuo, "Mwana-Kondoo amesimama, alikuwa kana kwamba amechinjwa," ametajwa (Ufunuo 5:6; 13:8).
- Anazitakasa dhamira zetu kutokana na matendo mafu, yaani, kuchana na dhambi (Waebrania 9:14).

**11. Je, ni lini ambapo lile hekalu la mbinguni lingetakaswa? Danieli 8:14.**

______________________________________________________________________

a) Mnamo 1844, pale hukumu ya upelelezi inapoanza.
b) Ni lazima litakaswe kwa kafara iliyo bora zaidi (Waebrania 9:23, 24).
c) Alizitwaa dhambi zetu juu Yake Mwenyewe, kama vile unabii usemavyo (Isaya 53).

## *HITIMISHO*

**12. Je, Yesu atatangaza nini pale anapokoma kufanya utetezi kwa ajili yetu na ile hukumu ya upelelezi inapofikia mwisho wake? Ufunuo 22:11.**

______________________________________________________________________

*Pale anapokitupa kile chetezo cha dhahabu hapa duniani (Ufu.8:5), hapatakuwako na uombezi tena kwa mwanadamu.*


**13. Maneno yetu, matendo yetu pamoja na mivuto yetu, vyote vitahukumiwa. Je, kutakuwako na nafasi ya pili kwa wale ambao hawatubu hivi leo? Yeremia 2:22.**

______________________________________________________________________

Huenda, yamkini hivi sasa ndipo hatima yako inaamriwa. Kiwango kinachoangaliwa katika hukumu ni ile sheria ya Mungu, ambayo twawezaa tu kuitii kwa njia ya nguvu za haki ya Kristo ndani yetu. Yesu anatamani sana kutuhesabia sisi haki, kututangaza kama watu tusio na hatia kwa njia ya sifa Zake. Kuna njia moja pekee: tujisalimishe Kwake kabisa. Je, utamkubali hivi leo kuwa wakili wako na kumpatia moyo wako?

**_Uamuzi wangu:_** *Ninaamini ya kwamba hukumu ya upelelezi ilianza mwaka 1844 na ya kwamba Kristo aliingia katika Patakatifu Mno pa hekalu la mbinguni.* ❑ *Ndio* ❑ *Hapana*

# 23 JE, NI KWA NINI KUNA DINI NYINGI?



Watu wengi hujiuliza wenyewe swali hili pale wanapoona ya kwamba:

- Kuna mamia ya makundi ya kidini na maelfu ya madhehebu. Kila kundi hudai ya kwamba linayo ile kweli, na walio wengi hufanya msingi wa mafundisho yao kutoka katika Biblia na kumwamini Yesu Kristo.
- Je, hawa wote ni kanisa la Mungu? Je, Bwana anayatambua makanisa haya yote kama wateule Wake, ama anao watu Wake maalumu? Iwapo ni hivyo, kanisa la Mungu lawezaje kutambulika?
- Katika kila dini, kuna watu waaminifu wanaompenda Mungu, lakini hili halimaanishi ya kwamba kanisa lile wanalohudhuria ndilo kanisa la kweli. Neno la Mungu, na hususani katika nabii mbali mbali, tunapewa vidokezo vitakavyotusaidia sisi kuwatambua masalio wa Mungu halisi.

## *MIFANO INAYOLIWAKILISHA KANISA*

**1. Je, kanisa la kweli linalinganishwa na nini, katika Agano la Kale na Agano Jipya pia? Isaya 5:1, 2, 7; Mathayo 21:33.**

_____________________________ *limezungushiwa kwa* _______________________________ .

*a) Ule mzabibu (Yohana 15:1, 2, 4): Kristo Ndiye shina la ule mzabibu. Yeye ni wa milele. Sisi tu matawi. Tukaapo ndani Yake tutazaa matunda, vinginevyo, tutakatiliwa mbali.*

*b) Ukuta: kusudi lake ni kuweka mpaka kati ya nchi ya Bwana na ile nyingine. Ukuta huu hulilinda kanisa maadamu linaendelea kuyafanya mapenzi ya Mungu. Ule ukuta unafananishwa na sheria ya Mungu.*

*Eneo lililo nje ya sheria ya Mungu ni dhambi (1 Yohana 3:4).*

*Kanisa lo lote ambalo linaiacha amri ya Mungu yo yote linatoboa tundu katika ule ukuta.*

**2. Katika Biblia yote kanisa linafananishwa na mwanamke (2 Wakorintho 11:2). Kulingana na Wimbo 6:8, 9; 4:7, je, ni makanisa mangapi ambayo Bwana anayatambua kama ni Yake?**

______________________________________________________________________________

**3. Je, unabii unasemaje juu ya wanawake (makanisa) wa nyakati zetu? Isaya 4:1.**

*a) Wanawake saba: hawa wote ni makanisa (7 inawakilisha ukamilifu).*

*b) Hawa wote wanamshikilia mwanamme mmoja: makanisa yote huzungumza juu ya Kristo.*

*c) Wanakula chakula chao wenyewe: wote wanayo mafundisho ya kwao wenyewe, badala ya neno la Mungu.*

*d) Wanavaa mavazi ya kwao wenyewe: kujihesabia haki wenyewe (Isaya 64:6), badala ya vazi la haki ya Kristo (Mathayo 22:11, 12). Wanaridhika kwa kuitwa tu kwa jina Lake: Wakristo (Ezekieli 33:31).*

## *KANISA LA MUNGU KATIKA UFUNUO 12*

**4. Mwanamke huyu anayeelezwa katika Ufunuo 12:1 anaonekanaje, naye anawakilisha nini?**

*a) Mwanamke huyu anafananishwa na kanisa la kweli. Alivikwa ________. Jua linamwakilisha Kristo, Jua la Haki (Malaki 4:2).*

*b) Na ______________ chini ya miguu yake. Huu unafananishwa na Agano la Kale, msingi wa nuru ya Kristo. Nyota 12 inawakilisha wanafunzi wale thenashara.*

**5. Kanisa hili liliahidiwa uzao, Mwokozi (Mwanzo 3:15). Mtoto huyu anamwakilisha nani? Ufunuo 12:2, 5.**

_________________________________________ *(Zaburi 2:7-9).*

- *"Kuumwa katika kuzaa": hapakuwa na nafasi katika Bethlehemu, Naye akazaliwa katika hori.*

**6. Kulikuwa na ishara nyingine, ni joka. Huyu anamwakilisha nani? Ufunuo 12:3, 4, 9.**

*Ulikuwa ni __________________________ uliojibainisha katika Dola la Rumi.*

- *Ulisimama mbele ya yule mwanamke ili amle mtoto wake; hii inahusu yale mauaji ya watoto yaliyoagizwa na Herode.*

**7. Je, ni wapi ambako mwanamke yule, kanisa, alikimbilia kutokana na mateso? Mstari 13-16.**

_________________________________________________________________________________

- *Katika zile Zama za Kati, waumini walilazimika kukimbia kutokana na yale mateso ya upapa nao walijificha katika sehemu za mbali, zisizo na watu.*
- *Yale mabawa yanawakilisha ile kasi ambayo kanisa lilipasa kwenda nayo.*

**8. Je, zile mamlaka za mateso juu ya wale waaminifu zingedumu hata lini? Mstari 6, 14.**

*Siku za kinabii ___________________________________________________________________*

- *Kipindi hiki pia kimetajwa kama nyakati tatu na nusu. Wakati mmoja ni sawa na siku 360, ambazo, ukizidisha kwa 3.5 unapata jumla ya siku 1,260. Kwa kulingana na ufunguo wa kinabii siku hizi 1,260 ni miaka halisi. Hiki kilikuwa ndicho kipindi cha enzi ya utawala wa kipapa, ambacho kilikuwa kati ya mwaka 538 hadi 1798, pale Papa alipotiwa akifungoni na Ufaransa.*

**9. Je, mateso haya pia yanaelezewaje, na ni jinsi gani kanisa lilivyosaidiwa? Mstari 15, 16.**

*Nyoka akatoa katika kinywa chake ________________________ kama gharika… nayo ____________ ikamsaidia mwanamke.*

- *Maji yanawakilisha umati wa watu (Ufunuo 17:15), waliotumwa ili kuwatesa wale waaminifu.*
- *Nchi ikamsaidia mwanamke: katika yale Matengenezo ya karne ya 16, serikali mbali mbali za Ulaya ziliyalinda maisha ya wale watu waliokuwa wakiteswa. Kugunduliwa kwa bara la Amerika kukawa ni msaada mkubwa, maadamu watu wengi waliweza kuondoka kutoka Ulaya na kujipatia hifadhi na uhuru kule.*



**10. Mwishoni mwa unabii tunamwona tena yule mwanamke, hii ikimaanisha watu wa Mungu katika ule mwisho wa wakati. Je, ni tabia zipi zitalionesha kanisa la kweli? Ufunuo 12:17.**

a) *Lingekuwa ni kanisa linaloteswa. "Joka … akaenda zake afanye vita juu ya …"*
b) *Lingekuwa ni masalio, watu wachache (Sefania 3:12).*
c) *WANGEZISHIKA AMRI ZA MUNGU.*
d) *Wangekuwa na ushuhuda wa Yesu, ambao ni roho ya unabii (Ufunuo 19:10).*

**11. Je, ni aina gani nyingine ya mwanamke ambayo kitabu cha Ufunuo kinaeleza? Ufunuo 17:1-6.**

*Anaitwa ______________________________ mkuu. Babeli humaanisha machafuko. Babeli anaainishwa kama kahaba kwa sababu anaruka na wafalme (wanasiasa) badala ya kuwa wa Kristo peke yake. Huyu siye mwaminifu Kwake (Yakobo 4:4); hii pia ilikuwa ndio dhambi ya Israeli (Isayan1:21, 22).*

a) *Utawala wake ni wa ulimwengu wote (maji, Ufunuo 17:15); makao yake makuu, Rumi, mji ulio juu ya vilima saba, (mstari 9); ile rangi nyekundu pamoja na utajiri wake katika dhahabu (mstari 4), yale mafundisho ya uongo anayoyafundisha (kikombe kilichojaa machukizo); pamoja na historia yake ya mateso (mstari 6) huonesha utambulisho wa kanisa hili.*
b) *Babeli ni mfumo wa kidini. Iwapo kuna kanisa-mama, pia kuna mabinti. Hawa ni nani? Makanisa yale ambayo kwa njia fulani huliigiza kanisa la Rumi. Kwa mfano, wanaadhimisha siku ya Jumapili, wanahubiri juu ya kutokufa kwa roho, ama kutokuwa na kipingamizi juu ya kushiriki katika vita.*

## *KANISA SAFI*

**12. Je, mafundisho ya kanisa hili, ambalo kichwa chake ni Kristo yanaelezwaje? Waefeso 5:23, 26, 27.**

______________________________________________________________________

**13. Kanisa la Mungu lingekuwaje? 1 Timotheo 3:15.**

______________________________________________________________________

## *HITIMISHO*

**14. Je, ni wito gani ambao Mungu anawapatia wale waaminifu waliomo katika Babeli, wale wote walio katika mfumo wa kidini potofu? Ufunuo 18:4.**

______________________________________________________________________

- Yesu anatuita sisi sote kuingia zizini, kuwa sehemu ya mwili ambao ni kanisa Lake.
- Watu wa Mungu wa kweli wana tabia ya utii juu ya amri Zake. Hebu na tuwe waaminifu kwa Yesu, kwa jinsi hii tukionesha upendo wetu Kwake. Hebu na tubaki katika lile shamba la zabibu lililozingirwa na ukuta wenye ulinzi, nasi tubaki tukiwa tumeungana na ule mzabibu ambao ni Yesu Kristo Mwenyewe ili kwamba tuweze kuzaa matunda mengi.

---

***Uamuzi wangu:*** *Ninaamini ya kwamba kanisa la kweli linajitambulisha lenyewe kwa sababu linazishika amri za Mungu.* ❑ *Ndio* ❑ *Hapana*

---

# 24 666 NA MAREKANI KATIKA UNABII




Tarakimu hii yaweza kumhusu nani?

Kuna nadharia pamoja na dhana nyingi juu ya mada hii. Wengine wanaihesabia tarakimu hii kwa Nero; na wengine kwa Hitler. Kuna vielelezo vinavyohusiana na umizimu na kupunga pepo. Wengine wanaunganisha tarakimu hii na mfumo potofu wa mahesabu. Ukweli wake uko vingine kabisa: mnyama huyu wa kimfano wa Ufunuo 13, ambaye tarakimu yake ni 666, ni mamlaka ile inayowakilishwa na ile pembe ndogo ya Danieli 7.

## *MNYAMA WA KWANZA WA UFUNUO 13*

**1. Mnyama huyu alitokea wapi, na ni maelezo gani yanayoonesha jografia ya eneo la makao yake makuu? Ufunuo 13:1, 2.**



*a) Aliinuka kutoka ______________. Hii inaonesha ya kwamba mamlaka hii ilitokea mahali penye wingi wa watu.*

*b) Alikuwa na vichwa ____________ na pembe __________. Ufunuo 17:9 inaeleza kwamba vile vichwa saba vinawakilisha vilima saba.*

*c) Mwili wa mnyama huyu ulifanana na wa yule chui, miguu yake ilifanana na ile ya dubu, na kinywa chake kilikuwa kama cha simba.*

*Wanyama hawa ni wale wale wanaowakilisha Uyunani, Umedi-Uajemi na Babeli katika Danieli 7.*

*Bila shaka, mnyama huyu wa Ufunuo 13 alikuwa na tabia kama zile zilizoshamiri katika falme zile zilizotangulia.*

**2. Mnyama huyu wa Ufunuo 13 alipokea nini kutoka kwa joka anayetajwa, kama alivyotajwa katika Ufunuo 12 (Shetani na Rumi ya Makaisari)? Ufunuo 13:2.**

*Yule joka akampa _____________________, na _______________________ , na uwezo mwingi.*

a) Mamlaka hii ingekuwapo hadi mwisho wa wakati, maadamu unabii huu unamtaja mnyama huyu katika pigo la tano (Ufunuo 13:9, 10; 16:10, 11).

b) Imetajwa kwa mara kadha kwamba ni Babeli (Ufunuo 14:8; 17:5; 18:2-4).

**3. Je, kuna ulinganifu gani kati ya mnyama wa Ufunuo 13 na ile pembe ndogo ya Danieli7?**

### *MNYAMA WA UFUNUO 13*

1. Alikuwa na kinywa kilichonena maneno makuu na makufuru (Ufunuo 13:5).
2. Akamtukana ____________ (mstari 6).
3. Alipewa kufanya vita dhidi ya watakatifu na
4. kuwashinda (mstari wa 7)
5. Ingefanya kazi yake kwa miezi 42, inayolingana na siku1,260 ama “wakati, nyakati mbili na nusu wakati” (Ufunuo 12:6, 14).
6. Akapewa uwezo juu ya kila kabila na jamaa na lugha na taifa (Ufunuo 13:7).
7. Angefanywa kuwa mateka na kuuawa kwa upanga (mstari wa 10).

### *PEMBE NDOGO YA DANIELI 7*

1. Ilikuwa na kinywa kilichonena mambo makuu (Danieli 7:8).
2. Atanena maneno kinyume chake
3. Aliye Juu (mstari 25)
4. Ilifanya vita na watakatifu na kuwashinda (mstari wa 21).
5. Walitiwa mikononi mwake kwa “wakati, na nyakati mbili na nusu wakati” (Danieli 7:25).
6. Ilikuwa hodari kuliko zile nyinginezo (mstari wa 20).
7. Hakimu angemwondolea utawala wake na kumwangamiza mwishoni (mstari wa 26).

***MAELEZO: Maneno ya makufuru na kunena kinyume chake Aliye Juu kunamaanisha nini?***

- Upapa unadai kusamehe dhambi, ambapo kwa hakika ni Mungu pekee awezaye kufanya jambo hili (Marko 2:7).
- Kwa kule kuitwa “Baba Mtakatifu,” papa anajipatia mwenyewe jina linalomhusu Mungu pekee (Mathayo 23:9).
- Anajifanya kuwa ndiye kichwa cha kanisa, na kwa jinsi hii kuichukua nafasi inayomhusu Kristo (Waefeso 5:23; 4:15).
- Akiwaruhusu watu kupiga magoti mbele yake ni tendo la sifa na kuabudu, ambalo linamhusu pekee Mungu. Petro hakumruhusu Kornelio kufanya hili (Matendo 10:25, 26), wala yule malaika hakumruhusu Yohana kufanya hivyo (Ufunuo 19:10; 22:8, 9).
- Kwa sababu hii, pale Paulo anaposema juu ya “yule mtu wa kuasi,” alisema ya kwamba huyu aliketi katika hekalu la Mungu, “akijionyesha nafsi yake kana kwamba yeye ni Mungu” (2 Wathesalonike2:3, 4). Neno hili mpinga Kristo linamaanisha yule aliye kinyume na Kristo, ama anayechukua mahali Pake.

**4. Je, ni jinsi gani pia ambavyo mnyama huyu anaweza kutambuliwa? Ufunuo 13:18.**

*Maana ni hesabu ya kibinadamu. Na hesabu yake ni ________________.*

*Katika Kilatini, ambayo ndio lugha rasmi ya upapa, herufi nyingi huwa na thamani ya kitarakimu. Tunapojumlisha thamani ya herufi hizi zilizo katika jina lililoandikwa katika taji yenye ngazi tatu ya Papa, VICARIUS FILII DEI, ambalo humaanisha Mwakilishi wa Mwana wa Mungu, tunapata matokeo yafuatayo:*



**“VICARIUS FILII DEI”**

**“MSAIDIZI WA MWANA WA MUNGU”**

**666**

**LATIN**

| | | |
|---|---|---|
| V | = | 5 |
| I | = | 1 |
| C | = | 100 |
| A | = | 0 |
| R | = | 0 |
| I | = | 1 |
| U | = | 5 |
| S | = | 0 |
| F | = | 0 |
| I | = | 1 |
| L | = | 50 |
| I | = | 1 |
| I | = | 1 |
| D | = | 500 |
| E | = | 0 |
| I | = | 1 |
| | | **666** |

**5. Je, kungetokea nini katika moja ya vichwa vyake? Ufunuo 13:3.**

*Kimetiwa ___________________ likapona. Dunia yote ikamstaajabia ________________ yule. (Ufunuo 13:5).*

*Katika kipindi kile cha siku za kinabii 1,260 ama miaka halisi 1,260 (Ezekieli 4:6) kufuatia tamko la Justinia mnamo mwaka 538 B.K., mateso makubwa yaliendeshwa dhidi ya Wakristo wasiokubaliana na kile kilichoitwa ‘‘Holy Inquisition’’ (Mahakama ya Kikanisa ya Kuwahukumu Wazushi wa kidini). Sio katika Ufaransa pekee, bali hata katika Uhispania na Ulaya yote, pia katika makoloni ya Amerika, Meksiko na Peru; zaidi ya watu milioni 50 waliteswa na kuuawa. Mnamo 1798, katika ile tarehe ambapo ile miaka 1,260 ilipoishia, mamlaka ile ikapata jeraha la mauti. Jenerali Berthier, kwa kufuata agizo la Napolioni Mtawala wa Ufaransa, alimchukua Papa Piusi VI mateka (Ufunuo 13:10), akalivunjilia mbali lile Tamko la Yustinia, akapokonya serikali za nchi tano ambazo upapa ulizimiliki katikati ya Utaliano, na kupokonya mamlaka za kisiasa alizokuwa nazo Papa. Ilionekana kana kwamba upapa usingepona kutokana na jeraha lile la mauti.*

**6. Kukatokea nini juu ya lile jeraha la mauti? Ufunuo 13:3, 4, 8.**

*Pigo lake la mauti __________________, na dunia yote ________________________________ .*

*Lile jeraha likapona. Kidogo kidogo, ule upapa ulianza kurejesha mvuto wake. Mnamo 1929, Benito Mussolini alitia saini mkataba pamoja na papa, akimpatia kiasi che ekari 44 ili kuunda serikali ya Vatikani. Ule umaarufu wa yule papa uliongezeka siku kwa siku pale alipowazuru Waprotestanti, watu wa nchi za Mashariki, Wakomunisti, na hata nchi za Umoja wa Mataifa. Kwa dhahiri, dunia yote humsujudia,*

*na kwa jinsi hii kumsujudia yule joka ambaye chini yake, papa ni chombo tu na ambaye kutoka kwake alipokea nguvu zake (Ufunuo 13:2-4).*

## *MNYAMA MWINGINE*



**7. Je, mnyama huyu mwingine alikuja kutoka wapi naye alifanana na nini? Ufunuo 13:11.**

a) Alipanda juu katika ___________________. Hakutoka katika bahari (kwenye wingi wa watu) bali kutoka mahali kwenye aghalabu wakazi wachache.

b) Alikuwa na pembe. Kwanza, alifanana na ___________ _________________, na tena akanena kama joka. Nyati ni mnyama aliye na tabia kama hizi, nayo ndio nembo ya nchi ya Marekani (nyati huonekana katika baadhi ya sarafu za Marekani).

**8. Je, unabii ulielezaje juu ya kuunganika kwa Marekani (Uprotestanti) pamoja na upapa (Ukatoliki)? Ufunuo 13:12.**

*Huyu angeifanya dunia na wote wakaao ndani yake ___________________________ mnyama yule wa kwanza ambaye jeraha lake la mauti lilipona.*

**9. Je, ni aina gani ya miujiza ambayo Uprotestanti pamoja na umizimu ungeifanya katika Marekani? Ufunuo 13:13, 14.**

________________________________________________________________________________

*Wengi watadanganywa na ishara hizi nao wataamini juu ya mfumo huu wa kidini, sanamu ya mnyama, kama ni ya Mungu hakika.*

**10. Je, ni kwa namna gani ambapo Uprotestanti katika Marekani ungeusujudu upapa, na ni kwa nini unaitwa kuwa ni sanamu ya mnyama? Mstari 14.**

- Kulingana na unabii katika Danieli 7:25 pamoja na hati za kihistoria zilizopo, tunafahamu ya kwamba ilikuwa ni upapa ambao uliamuru kuiadhimisha Jumapili kama siku ya pumziko, badala ya Sabato iliyotolewa katika Biblia. Uprotestanti uliikubali amri hii ya kibinadamu na kwa jinsi hii unauheshimu upapa na kuwa SANAMU yake, yaani, kitu fulani cha kufanana. Uprotestanti sio kwamba unalo jambo la kuiadhimisha Jumapili pekee kama jambo la pamoja na Ukatoliki bali wanashirikiana katika mafundisho ya kutokufa kwa roho na kujiunga katika mambo ya siasa na vita.

**11. Je, Uprotestanti, kwa njia ya mapatano pamoja na serikali ya Marekani, watajaribu kufanya nini juu ya masalio waaminifu? Ufunuo 13:15-17.**

*Wasiweze ____________________________ wala ____________________________________ .*

*Kadiri vile Rumi ilivyotumia nguvu za kisiasa katika kuwatesa hawa wachache wasiokubaliana nao, kipindi kitakuja ambapo serikali ya Marekani itatoa sheria ambazo zitahimiza uadhimishaji wa Jumapili, na adhabu kubwa zitawekwa juu ya wale wanaotunza Sabato.*

**12. Chapa ya mnyama iliyoajwa katika Ufunuo 13:16 ni nini?**

- Muhuri ya Mungu ni Sabato takatifu (Ezekieli 20:12, 20).
- Kanisa Katoliki linasema ya kwamba Jumapili ni ishara ya mamlaka yake.

## *UJUMBE WA MALAIKA WATATU WA UFUNUO*

**13. Je, malaika wa kwanza, mwenye injili ya milele, anayaita mataifa, kabila, lugha na jamaa zote wafanyeje? Ufunuo 14:6, 7.**

_______________________________________________________________

- *Kumtukuza Mungu kwa kuitambua neema Yake iokoayo na kuziheshimu amri Zake (Mhubiri 12:13).*
- *Ujumbe huu hutuonesha sisi ya kwamba tunaishi katika wakati wa hukumu ya upelelezi (kuanzia 1844) na ya kwamba ni lazima tumwabudu Muumba. Kwa jinsi gani? Kwa kuitakasa Sabato, ambayo ni siku ya uumbaji na muhuri ya Mungu.*

**14. Malaika wa pili alitangaza nini? Ufunuo 14:8.**

*Umeanguka, umeanguka* _______________________________________________ .

*Watu wa kweli wa Mungu, wanaowakilishwa na malaika huyu, wanayahubiri makanisa yote ya uongo (Babeli).*

**15. Je, ni onyo gani la kuogofya na muhimu alilolitoa malaika huyu wa tatu? Ufunuo 14:9-11.**

_______________________________________________________________

## *MUNGU ATAWAOKOA WATOTO WAKE*

**16. Je, ni kwa maneno gani ambavyo mtume anaeleza juu tabia ya kanisa la Mungu la Masalio, lililo na ujumbe makini kwa wakati wetu? Ufunuo 14:12.**

_______________________________________________________________

*Tangia mwanzo kabisa, kumekuwako na ushindani kati ya nuru na giza, kati ya kweli na uongo. Kadiri ule ujio wa Yesu unavyokaribia, Shetani ataongeza ghadhabu yake juu ya wale masalio wa Mungu wazishikao amri Zake. Lakini Yeye aliyemshinda Shetani pale msalabami atakuwa ndio msaada wa waumini katika zile nyakati ngumu za majanga ya mwisho. Yesu anatuita sisi hivi leo kufanya msimamo wenye maamuzi ya kusimama upande Wake ili kuipokea muhuri ya Mungu.*


---

***Uamuzi wangu:*** *Ninakubali ya kwamba ujumbe wa malaika watatu ndio wito wa mwisho wenye upendo ambao kanisa la Mungu litautoa kwa ulimwengu unaoangamia katika uovu.*

❏ *Ndio* ❏ *Hapana*

---

# 25 SIKU ILIYO MUHIMU ZAIDI KATIKA MAISHA YA MTU



Je, ni ipi siku iliyo muhimu zaidi katika maisha ya mtu?

Kwa wengine, ni ile siku waliyozaliwa; kwa wengine, ni siku ile walipohitimu masomo yao; kwa mgeni anayetembea katika nchi ya nje, ni siku ile alipopata uraia mpya na kuweza kujiimarisha katika nchi hiyo mpya; kwa wengi, ni ile siku ya ndoa yao.

Je, ni siku ipi ambayo Mungu huiona kama ni muhimu zaidi katika maisha yetu?

Ni siku ile ambayo hakika huunganisha yote katika matukio yaliyopo hapo juu: kuzaliwa, kuhitimu, uraia, ndoa, kifo, ufufuo, na maisha ya furaha zaidi. Ya kwamba haya yote yawezekana katika siku moja?

## *FAIDA YA KUZALIWA UPYA*

**1. Je, ni masharti gani ambayo Yesu alimweleza Nikodemu, kiongozi katika Israeli, yaliyo muhimu ili kuingia katika ufalme wa Mungu? Yohana 3:1-4.**

______________________________________________________________________

**2. Je, ni tabia gani tulizozaliwa nazo? Ayubu 15:14-16.**

______________________________________________________________________

a) Tunaishi katika tamaa za mwili wetu (Waefeso 2:3), na matunda yetu ni huzuni (Wagalatia 5:19-21).

b) Wale wanaoishi kwa kuufuata mwili, pasipo kuzaliwa upya, hawawezi kumpendeza Mungu (Warumi 8:7, 8).

c) Tunastahili kufa (Warumi 3:23; 6:23).

**3. Twawezaje kuzaliwa mara ya pili? Yohana 3:5.**

*Kwa* ___________________________ *na kwa* __________________________.

***a) Kuzaliwa mara ya pili inamaanisha:***

- Kumpokea Yesu katika maisha yetu, na kubadilisha mawazo na hisia zetu (Ezekieli 36:26 27).
- Neno la Mungu lifanye kazi ndani yetu kwa njia ya Roho Mtakatifu (1 Petro 1:23).
- Paulo alikuwa nao ujuzi kama huo (Wagalatia 2:20).

***b) Kuzaliwa kwa maji*** kunamaanisha kubatizwa, kufanya agano pamoja na Mungu, ushuhuda mbele ya uma wa maisha mapya (1 Petro 3:21).

**4. Je, ni mfano gani alioutoa Yesu katika Mto Yordani? Mathayo 3:13-17.**

______________________________________________________________________

*Je, ni kwa nini Yesu alibatizwa? Hakuwa na dhambi yo yote, hata hivyo alifanya hivyo ili kuwa mfano wetu.*

**5. Je, aliwaagiza wanafunzi Wake wafanyeje? Mathayo 28:19, 20.**

*Walitakiwa* ______________ *kwa jina la* __________*, na* _____________ *na* ____________________.

## *NI NJIA IPI ILIYO YA KIBIBLIA: KUNYUNYIZA AMA KUZAMISHA?*

**6. Je, ubatizo unaashiria na kukumbusha nini? Warumi 6:3-6.**

a) Unakumbusha juu ya ________________, ___________________, na ___________________ kwa Kristo.

b) Ni mfano wa kifo na kuzikwa kwa “utu wa kale” wa dhambi.

c) Unawakilisha ufufuo kwenye “maisha mapya.”

d) Unafananaisha utakaso wa kimbingu kutoka dhambini (Matendo 22:16).

*Ni ishara ya nje juu ya badiliko lililofanyika ndani ya moyo wa mtenda dhambi kwa njia ya neema ya Mungu. Kunyunyiza hakuwakilishi kile Mungu alichokisema kama ndio maana ya ubatizo. Ubatizo wa kweli hufanyika kwa njia ya kutoswa maadamu inaashiria kuzika.*

**7. Neno ubatizo linamaanisha nini?**

*Neno hili la Kiyunani humaanisha **“kutosa”** na wala sio kunyunyiza. Elimu ya mambo ya kale imethibitisha ya kwamba batizo zote katika karne za mwanzo zilisimama kwa kumbatiza muumini kwa njia ya kutoswa. Msafiri aweza kuona bado batizo kama hizi katika jimbo la Negevu, Thesalonika, Efeso, Rumi, Pisa na sehemu nyinginezo.*

**8. Je, kuna ushahidi gani ya kwamba ubatizo ulifanywa kwa kutosa? Matendo 8:36-39.**

*Baada ya Filipo kutoa ujumbe kwa yule Mkushi ndipo kisha aliomba kubatizwa, hapo wote wawili wakashuka majini na kisha kupanda kutoka huko. Na tunaposoma juu ya ubatizo wa Yesu tunasoma pia ya kwamba hawa walishuka majini na kisha walipanda kutoka huko. Iwapo ubatizo ulipata kufanywa kwa njia ya kunyunyiza, wasingepaswa kuteremka kule mtoni.*

## *JE, NI NINI KITANGULIE UBATIZO?*

**9. Mwanafunzi anapasa kuelekezwa kikamilifu. Je, Yesu kwa dhahiri alisema afundishweje? Mathayo 28:19-20.**

__________________________________________________________________

**10. Je, mtu yule anayebatizwa anataka kuokolewa kwa sababu gani? Marko 16:16.**

__________________________________________________________________

**11. Je, tunapasa kuzionaje dhambi zetu? Matendo 2:38.**

__________________________________________________________________

*Kutubu ni kuwa na sikitiko la kweli kwa ajili ya dhambi na kujaribu kugeuka kuiacha. Kabla hatujabatizwa, tunapasa kuziungama dhambi zetu na kuziacha. Tunapasa kuwa tayari kufa juu ya dhambi na kuishi kwa Mungu (Warumi 6:11). Je, yule aliyezaliwa mara ya pili aweza kuyatimiza haya yote? Huenda isiwe hivyo!*

**12. Je, tunaingia kanisani Mwake kwa mlango gani, ambalo ndio mwili wa wa Kristo? 1 Wakorintho 12:13, 27.**

__________________________________________________________________

*Kama vile ndoa ilivyo ni utimilizo wa tamko la upendo wa mwanamme na mwanamke, vivyo hivyo ubatizo ni tamko la upendo wa aliye mtoto wa Mungu. Yesu aliuonesha upendo Wake mkuu pale Kalvari. Ubatizo ni onesho la wazi la kujisalimisha, upendo, na uaminifu kwa Yesu.*

## *MEZA YA BWANA, AGIZO LILILOTOLEWA NA YESU*

**13. Kwani ile divai na mkate huwakilisha nini? 1 Wakorintho 11:23-26.**

a) Mkate huwakilisha ____________ Wake.

b) Ile divai hutukumbusha sisi juu ya _____________ aliyoimwaga kwa ajili yetu.

c) Agizo hili n liadhimishwe kwa ukumbusho Wake, maadamu linatukumbusha juu ya kifo Chake.

d) Hutangaza juu ya kuja Kwake kwa mara ya pili.

**14. Je, ni kipi kifanyike kabla mtu hajashiriki katika Meza ya Bwana? Mstari 28, 29.**

________________________________________________________________________

**15. Je, Yesu aliamuru nini kifanyike katika tukio lile la Chakula cha mwisho? Yohana 13:4-15.**

*Adhimisho la ________________________________ miguu. Ni kanuni ya unyenyekevu.*

## *HITIMISHO*

Ile kafara ya Kristo itakumbukwa na wote kwa milele zote (Mathayo 26:29). Alama za kusulubiwa Kwake zitabaki kuwa ukumbusho wa gharama iliyolipwa kwa ajili ya ukombozi wetu (Habakuki 3:4). Kule kubatizwa na kisha kwa nyakati kufanya kumbukizi ya kifo Chake kwa njia ya Meza ya Bwana, ndio njia aliyoitoa Yesu na kutupatia sisi neema Yake na kushiriki katika kafara Yake (Yohana 3:5).

---

***Uamuzi wangu:*** *Nataka kujiandaa kwa ajili ya kufanya agano pamoja na Mungu kwa njia ya ubatizo wa Kibiblia.* ❑ *Ndio* ❑ *Hapana*

---

# 26 NAMNA YA KUMTAMBUA NABII WA KWELI



Siku moja tutaweza kukabiliana na swali lile Paulo alilomuliza Mfalme Agripa: "Je! Wawaamini manabii? Najua ya kuwa wawaamini." (Matendo 26:27). Hata hivyo, mara zote tunamwonea mashaka mtu yule anayedai kuwa anao ujumbe kutoka kwa Mungu. Twawezaje basi kumbainisha yule aliye wa kweli na mwongo?

Katika muda wote, Mungu amewaongoza

## *MUNGU HUWASILIANA NA MWANADAMU*

1. **Hapo mwanzo, Mungu aliwasiliana na mwanadamu ana kwa ana, lakini dhambi ikamtenga mwanadamu kutoka kwa Mungu (Isaya 59:2). Kristo akafanya daraja kati ya mwanadamu na Mungu. Je, ni njia gani ambayo Mungu aliitoa ili kuzifunua siri Zake kwa wanadamu? Amosi 3:7.**

   ______________________________________________________________________

   *Wale manabii walizungumza kadiri walivyosukumwa na Roho Mtakatifu (2 Petro 1:21).*

2. **Je, kuwa nabii kunakuja kama cheo cha kibinadamu, kwa kurithi, ama huja moja kwa moja kutoka kwa Mungu? Waefeso 4:8, 11.** ______________________________

3. **Je, nabii ni nani?**

   *Neno hili nabii hutokana na maneno mawili ya Kiebrania: roeh linalomaanisha kuona; ndio maana nabii huitwa pia kama mwonaji (1 Samweli 9:9), na neno jingine nabii, linalomaanisha kutamka. Kwa hiyo, nabii huona na kutangaza kile Mungu alichomwonesha na kisha huuandika ule ujumbe (Danieli 7:1). Husimulia juu ya matukio yajayo, kwa kulingana na mafunuo na mapenzi ya Mungu.*

4. **Je, Mungu huwasilishaje jumbe Zake kwa manabii? Hesabu 12:6-8.**

   ______________ *kwa* _________________*: njia hii ilitumika kwa Musa pekee.*

   *Katika* ___________________*: na macho yaliyofumbuliwa, bila ya pumzi, nabii huyu huyaona mambo katika mfuatano wa yale Mungu anayomwonesha kuhusu wakati uliopita, wakati uliopo, na wakati ujao, pamoja na matukio yalivyo katika ulimwengu usioonekana.*

   *Kwa njia ya ndoto za kinabii: njia hii isiwachanganye na zile ndoto nyingine za kawaida, ambazo huja kutokana na yale yanayoingia akilini ya kawaida, yasiyo dhahiri (Mhubiri 5:7). Kulikuwako na manabii katika nyakati za Agano Jipya na Agano la Kale pia. Wengi hupotosha fungu la Mathayo 11:13 na kufikiri kwamba baada ya Yohana Mbatizaji kusingekuwako na manabii zaidi. Hata hivyo, twaweza kuona kwamba kulikuwako na manabii wengine baada ya Yohana: Agabo (Matendo 21:10), Anna (Luka 2:36), Simoni (Matendo 13:1), na wengine. Paulo, Petro na Yuda pia walitoa unabii.*

5. **Je, ni aina gani ya manabii watakaoinuka katika mwisho wa wakati? Mathayo 24:24.**

   ______________________________________________________________________

**6. Je, kusudi la Mungu katika kuwapatia watu Wake kipawa cha unabii ni nini? Waefeso 4:11, 12.**

_____________________ *watakatifu, kuwaonesha makosa yao na kuwaonya.* _______________ *mwili wa Kristo kwa kuonesha maajabu ya mpango Wake wa ukombozi pamoja na matukio yajayo. Ili kusaidia kuleta umoja katika imani, kwa wazi kuyaonesha matakwa ya Mungu.*

**7. Kwa kulingana na kitabu cha Ufunuo, je, kanisa hili la mwisho lingekuwa na kipawa hiki cha unabii? Ufunuo 12:17; 19:10.**

*Ushuhuda wa Yesu ni* _______________________________________________________ .

**8. Twawezaje kumbainisha nabii wa kweli kutokana na yule wa uongo?**

## *TABIA KUMI ZA NABII WA KWELI:*

1. Maisha yake yatakuwa ni ya mfano (Mathayo 7:15, 16). "Mtawatambua kwa matunda yao." Matokeo ya kazi zake yatathibitisha juu ya asili yake ni ya mbinguni.
2. "Na waende kwa sheria na ushuhuda" (Isaya 8:20). Mafundisho yake yataafikiana na sheria ya Mungu pamoja na ujumbe wa manabii waliotangulia.
3. Unabii wote anaouhubiri utokee kwa dhahiri (Kumbukumbu 18:22).
4. Wala hashawishi uasi ama kujitenga na kusudi la Mungu (Kumbukumbu 13:1-4).
5. Anakubaliana na kufanyika mwili kwa Kristo (1 Yohana 4:1-3).
6. Ujumbe wake ni lazima uwe mnyofu. Hatakuwa wa kujisifu; badala yake, anaonesha dhambi za watu (Isaya 58:1), na hukumu za Mungu zilizo karibu sana (Ufunuo 14:6, 7).
7. Ujumbe wake ni wa makini, sio wa hivi hivi tu. Anachangia katika ukuaji wa kiroho wa kanisa na kutoa ushauri juu ya masuala ya kidini (2 Wakorintho 13:2, 3).
8. Mafundisho yake na maisha yake yatakuwa na Kristo kama chimbuko lake (2 Wakorintho 10:5).
9. Atatoa unabii kwa jina la Bwana naye wala hatatoa fasiri za kwake mwenyewe (2 Petro 1:20, 21).
10. Tunapasa kuangalia kama ni kwa jinsi gani anapokea maono hayo na uhusiano wake na watu wa wakati wake (Danieli 10:8).

## *KIPAWA CHA UNABII NA MWANAMKE*

**9. Je, mwanamke aweza kuwa na kipawa cha unabii? Biblia inawataja:**

*a) Miriamu (Kutoka 15:20)  b) Debora (Waamuzi 4:4)  c) Hulda (2 Wafalme 22:14)*
*d) Anna (Luka 2:36)  e) Binti wanne wa Filipo (Matendo 21:9).*

**10. Je, kipawa hiki kimedhihirika katika kanisa la Mungu katika hizi nyakati za mwisho?**

*Mnamo 1844, wakati ambapo kwa kulingana na unabii ule, ukweli ambao ulikuwa umekanyagwa mavumbini kuwa ungerejeshwa, Mungu akatuma ujumbe kwa watu Wake kwa njia ya Roho ya Unabii. Ellen Harmon, ambaye alikuja kujulikana kama Ellen G. White, akiwa msichana dhaifu mwenye umri wa miaka 17, alikuwa ni chombo cha maana mkono Mwake Mungu. Huyu alizitimiliza zile tabia kumi tulizotangulia kuzitaja. Wale wanaoyasoma maandishi yake wanaona ya kwamba yanafanya kazi ya kuimarisha makuzi ya kiroho ya kanisa na kuhamasisha umoja wa kiimani. Licha ya kuwa elimu yake ilikuwa ni ndogo, aliweza kuandika zaidi ya kurasa 100,000 zilizochapishwa katika zaidi ya vitabu 50 ambavyo vinaendelea kusambazwa hata leo, sambamba pamoja na mamia ya majarida, na kiasi cha mada zipatazo 4000 zilizoandikwa katika magazeti kadha. Wasomi wa kidini wanatambua ya kwamba maandishi yake yamevuviwa. Huyu alipokea mafunuo, akayaandika, na kuyahubiri kwa mamilioni ya watu tokea 1844 hadi 1915, ambacho ni kiasi cha zaidi ya miaka 70. Watu wengi wameshuhudia ya kwamba aliishi maisha ya kimfano. Katika kila wakati, alimwinua Yesu Kristo kama ndiye chimbuko na alimwonesha katika namna ya pekee sana; pia aliiinua ile sheria takatifu ya Mungu. Matabirio yake yalikuja kutimilika yote kwa usahihi kabisa, haya ni pamoja na kutokea kwa Vita*

*Kuu ya Kwanza ya Dunia, kuangamia kwa meli pamoja na majumba makubwa, pamoja na mioto ambayo hapana mtu aliyeweza kuizima; kuharibiwa kwa miji ya San Francisco na Oakland kule California Marekani katika tetemeko la nchi la 1906; kuongezeka kwa imani za rohoroho (mizimu) pamoja na muungano wa Wakatoliki pamoja na Waprotestanti; pasipokuwa na elimu ya kimsingi katika taaluma ya elimu ya nyota, yeye alitoa kwa usahihi kabisa mambo ya hakika ya taaluma hiyo ya nyota, alitoa pia maelekezo ya kisayansi juu ya afya, kama vile mivuto inayotawala kabla ya kipindi cha balehe. Zaidi ya hayo, ameeleza juu ya chanzo cha saratani, lishe, n.k. Katika maandishi yake yaliyo mengi, hayana upinzani wo wote na Biblia. Maandishi yake ni kama vile darubini; hayapingani bali kupanua maelezo. Pia yanakuwa kama vile ni kiona mbali ambacho hakizui nyota mpya bali kuonesha uzuri wa zile zilizopo. Baadhi ya vitabu vyake ni: Steps to Christ (Njia Salama) [kilichochapishwa katika lugha zaidi ya 100], The Great Controversy (Pambano Kuu), The Desire of Ages (Tumaini la Vizazi Vyote), The Ministry of Healing (Huduma ya Uponyaji), Patriachs and Prophets (Mababu na Manabii), Patriachs and Kings (Mababu na Wafalme), Child Guidance, Testimony Treasures, n.k. Kiini kikuu cha ujumbe wa Ellen White kilikuwa ni maisha ya Kristo-Kufanyika Kwake kuwa mtu, huduma Yake, kifo, kufufuka pamoja na kazi Yake ya hivi sasa kwa niaba ya mwenye dhambi pale katika hekalu la mbinguni. Tukitazama katika maisha ya Yesu Kristo yaliyopata kuandikwa yanapatikana katika vitabu vyake: Njia Salama na Tumaini la Vizazi Vyote, miongoni mwa vinginevyo, vitabu ambavyo tunashauri visomwe.*

## *HITIMISHO*

**11. Asante sana kwa msaada huu wa kimbingu, tunapata uelewa wa kina zaidi juu ya njia za Mungu. Je, kunatokea nini kwa watu wa Mungu wawapo bila ya neno la unabii? Mithali 29:18.**

__________________________________________________________

**12. Je, Mungu anatupatia ushauri gani? 1 Wathesalonike 5:20, 21.**

__________________________________________________________

*Neno la Mungu linasema ya kwamba kanisa la mwisho litakuwa na kipawa cha unabii. Iwapo mafunuo haya yasingekuwako, tusingezifikia sifa zinazohitajika za kanisa la kweli.*

**13. Je, kipawa hiki ni muhimu hata lini? Waefeso 4:13.**____________________________

**14. Je, Mungu anawaahidi nini wale wanaowaamini manabii hawa? 2 Nyakati 20:20.**

__________________________________________________________

***Uamuzi wangu:*** *Ninaamini ya kwamba Mungu alijifunua mwenyewe kwa kanisa la mwisho kwa njia ya roho ya unabii.* ❑ *Ndio* ❑ *Hapana*

# 27 FUNGUO SABA ZA KUFIKIA KWENYE MAISHA YA KIAFYA



Mungu anataka tuwe wenye afya na kuishi wenye furaha. 3 Yohana 2.

- Furaha yetu inahusiana sana na afya yetu.
- Ni lazima tuwe waangalifu juu ya miili yetu, kwa sababu Mungu anatuchukulia sisi kama hekalu Lake. 1 Wakorintho 6:19, 20.
- Mungu anataka kutupatia hekima ili kwamba tuweze kuepa magonjwa ama kupona kutokana na kuumwa.

1. **Biblia inasema ya kwamba mwili wetu ni hekalu la Roho Wake Mtakatifu. Je, Mungu atafanya nini juu ya wale ambao kwa hiari wanaliharibu hekalu? 1 Wakorintho 3:16, 17.**

______________________________________________________________________

**Tunapotafakari juu ya wajibu wetu mkuu katika kuitunza miili yetu, hebu na tuviangalie vipengee hivi saba muhimu. Tunapotafakari juu ya wajibu wetu mkuu katika kuitunza miili yetu, hebu na tuviangalie vipengee hivi saba muhimu:**

- ***Moja:*** Tumia maji ndani na nje ya mwili. Madaktari wanashauri kutumia glasi sita hadi nane kwa siku, yanywewe katikati ya milo, ili kuusafisha mfumo wa mwili. Kuoga kwa kila siku pia ni jambo la faida sana, maana kunausisimua mfumo wa uondoaji wa sumu mwilini kwa njia ya vinyweleo, kwa jinsi hii kunachangia kuboresha afya ya mwili.
- ***Mbili:*** Pumzika vya kutosha. Tulale angalau kwa saa 8 kwa siku (japo watoto wanahitaji muda zaidi) kwa sababu ndipo mfumo wa neva unapoimarishwa. Zaidi ya hapo, kuwa na siku ya kupumzika ya juma, ndio Sabato, ni baraka kwa mwili na roho.
- ***Tatu:*** Timiliza mazowea fulani. Jiwekee ratiba ya milo. Kula katikati ya mlo na mlo hulilemea tumbo. Tunapomaliza kula, na tulipumzishe tumbo kwa saa kama nne hadi sita, pasipo kuingiza kitu kingine tena ila vinywaji.
- ***Nne:*** Jizoeshe kuwa na kiasi. Unapasa kuwa na kiasi wakati ulapo, kazini na katika shughuli zote: kijinsia, kiakili, n.k. Hata kile chakula chenye afya zaidi, kikiliwa kwa kuzidisha kinaweza kuwa chenye madhara kwa afya yetu. Tuachane na mawazo ya kwamba tuwapo mezani tungekula zaidi. Umeng'enyaji wa chakula huanzia kinywani, kwa hiyo unapasa kutafuna chakula chako vizuri. Kiasi humaanisha kuwiana. Tusile kwa sababu tu tunapenda chakula fulani bali pia ya kwamba ni chema kwetu.
- ***Tano:*** Ule vyakula vya asili. Tutalifafanua hili hapa chini:

2. **Je, ni chakula cha aina gani alichopewa mwanadamu pale alipoumbwa kule Edeni? Mwanzo 1:29.**

______________________________________________________________________

*Matunda, mimea iliyo na mbegu ndani yake, pamoja na nafaka vilikuwa ndio chakula alichopewa mwanadamu pale mwanzo.*

3. **Je, ni lini pale mwanadamu alipopewa namna fulani ya nyama, zilizoitwa nyama safi? Mwanzo 7:2; 9:3, 4.**

______________________________________________________________________

*Kabla ya ile gharika, kiasi cha miaka 1,500 baada ya uumbaji, watu wa Mungu hawakula nyama. Walikuwa ni watu walioishi kufikia hata miaka 500; lakini mara baada ya nyama kuruhusiwa katika chakula cha mwanadamu, ule umri mrefu mara ukapungua.*

*Ijapokuwa mwanadamu aliruhusiwa kula nyama baada ya gharika, kamwe hakuruhusiwa kula damu, mafuta pamoja ama nyama najisi. Aliweza tu kula aina ya wanyama waliotajwa katika Walawi 11 na Kumbukumbu 14.*

**4. Wana wa Israeli walipokuwa jangwani kuelekea Kanaani, Nchi ya Ahadi, Mungu alitaka kuwapatia chakula maalumu bila ya nyama. Je, walikutana na adhabu gani kwa kutotaka kutii maagizo ya Mungu? Hesabu 11:4, 19, 20, 33, 34.**

______________________________________________________________

**5. Je, ni nani ambao wangejifunza kutokana na mfano huu uliopo hapo juu, na ni amri gani ambayo Bwana anawapatia watu wanaoishi katika wakati huu wa mwisho? 1 Wakorintho 10:5. 6, 11.**

______________________________________________________________

*Kusudi la Mungu lilikuwa kwamba watu Wake warejee kwenye chakula chenye kuleta afya alichopewa mwanadamu pale mwanzoni mwa ulimwengu; matunda, njugu, mboga mboga, pamoja na nafaka; milo ya asili bila ya nyama.*

**6. Je, nyama itakuja kuliwa mbinguni na katika umilele? Ufunuo 21:4; Isaya 25:8.**

______________________________________________________________

*Matunda matamu ambayo hukua kila mwezi yataliwa (Ufunuo 22:2). Kile chakula alichopokea mwanadamu katika paradiso, ambacho kilikuja kubadiliwa na dhambi, kitarejeshwa pale Yesu ajapo.*

**7. Je, Danieli pamoja na rafiki zake walipata manufaa gani kutokana na kuepuka ulaji wa nyama pamoja na vinywaji vya ulevi? Danieli 1:8-20.**

______________________________________________________________

**8. Je, kuna faida zipi katika vyakula vya mboga na maziwa?**

| KIMWILI: | KIMAADILI: | KIROHO: |
|---|---|---|
| a) Pungufu mara kumi katika hatari ya magonjwa ya kuambukiza. | a) Kuwa na huruma juu wanyama. | a) Kupungua kwa hatari zenye kudhoofisha hisia safi za akili zetu. |
| b) Kuliwa kwa kiasi kidogo zaidi kwa kolestro, na hivyo kuepukana na magonjwa ya mishipa ya moyo. | b) Kuwa na mwelekeo pungufu kwenye kufanya maasi na kutumia nguvu sana. | b) Kiasi na kujistahi. |
| c) Kuliwa kwa kiasi kidogo zaidi vyakula vinavyokuja kutengeneza asidi mwilini, na hivyo kuepukana na magonjwa ya baridi ya bisi na yale yanayoshambulia mifupa. | c) Kuwa na upungufu wa wepesi wa hasira, maadamu nyama huwa na vichocheo. | c) Kuwa na hali ya kiroho zaidi. |
| d) Kuwa na mfumo mzuri wa umeng'enyaji wa chakula tumboni na kupunguza hatari ya kupata saratani. | d) Hisia za maadili hazidhoofishwi. | d) Viumbe walioumbwa na Mungu hawauawi kwa kuridhisha uchu wetu wa chakula. |

**KIMWILI:**

e) Kuepuka homoni, chanjo, na madawa anayopewa mnyama yasiingie mwilini mwangu.

f) Kuwa na kinga zaidi kwa vile mwili haujajawa na sumu mbali mbali.

g) Kuwa na maisha marefu zaidi.

**KIMAADILI:**

e) Gharama pungufu, na watu zaidi waweza kulishwa.

f) Huepuka mielekeo ya ngono za jinsia moja, ambazo kwa sehemu hutokana na vyakula vyenye homoni zilizochochewa.

g) Kuwa na huruma zaidi juu ya wengine.

**KIROHO:**

e) Hakuna hatari ya kula damu za wanyama, ambazo Mungu amekataza.

f) Tunamtukuza na kumsifu Mungu tunapoilinda miili yetu.

g) Tunarejea kwenye mfumo asilia wa chakula, hivyo tunatimiliza mpango wa Mungu kwa wakati wetu.

➢ ***Sita:*** Epuka vyakula vilivyokolezwa na madawa.

- Tumbaku ni muuaji asiye na rehema wa mamilioni ya watu. Mmoja katika wavuta sigara watano hufa kwa saratani. Wala tusiuharibu mwili wetu, kwa sababu ni hekalu la Mungu (1 Wakorintho 3:16, 17).

**9. Je, Biblia inasema nini juu ya utumiaji wa vinywaji vyenye kileo? Mithali 20:1; 23:29-33.**

____________________________________________________________

**10. Je, ni aina gani ya chakula ambacho Yohana Mbatizaji, aliyeiandaa njia ya ujio wa kwanza wa Yesu alikitumia tokea akiwa tumboni mwa mama yake? Luka 1:15.**

____________________________________________________________

*Kwa kadiri tunavyoiandaa njia kwa ajili ya ujio wa pili wa Kristo, je, unafikiri ya kwamba chakula chetu sio muhimu sana hivi sasa kuliko ilivyokuwa katika siku zile?*

**11. Je, ni vichocheo gani vingine vinavyodhuru afya yetu?**

- Kahawa, chai, pamoja na vinywaji vyepesi vyote vilivyo na kafeini (mateini na theini vyote ni sawa), ambazo hudhuru mfumo wa fahamu na kuleta maumivu ya mwili. Hivi vyote tunapasa kuviepuka.
- Madawa kama vile LSD, morfaini, bangi, kokeini, pamoja na baadhi ya madawa yanayoufanya mwili kuugua, huharibu akili, kuidhalilisha nafsi, na kumwudhi Muumba wetu.

➢ ***Saba:*** Kutumia madawa ya kiasili, na kuwomba Mungu atusaidie.

**12. Je, mimea imeumbwa kwa kusudi gani? Zaburi 104:14.**

____________________________________________________________

*Yesu alitumia tope ili kumponya mtu yule kipofu, Naye akashauri kutumia maji (Yohana 9:6-12). Mfalme Hezekia aliponywa kwa kutumia mkate wa tini (2 Wafalme 20:5-7), ikionesha ukubali wa Mungu juu ya njia za kiasili katika uponyaji.*


**13. Nasi tungefanyeje pale tunapougua? Yakobo 5:14, 15.**

____________________________________________________________

*Biblia inasema kwa mapema ya kwamba kutakuwako na miujiza mingi ya uongo pamoja na maajabu katika wakati huu wa mwisho. Kunaweza kuwako na wokovu pasipo uponyaji na uponyaji pasipo na wokovu. Wengi watajikuta wamedanganywa katika ile hukumu ya mwisho (Mathayo 7:21-23).*

*Hebu na tukamtukuze Mungu katika miili yetu (1 Wakorintho 10:31). Bwana Yesu, katika upendo Wake usio na mfano, aliyatoa maisha Yake ili kuniokoa mimi; je, inafaa mie nipuuzie kuutunza mwili huu, ambao Yeye aliuumba na tena akaufia?*

# LISHE: EDENI HADI EDENI



**14. Je, ningefanyeje katika kuitikia upendo Wake huu? Warumi 12:1, 2.**

______________________________________________________________________

*Iwapo wale wanaotafuta utukufu wa dunia hii katika michezo huwa makini katika kuitunza miili yao, je ni zaidi kiasi gani ambavyo sisi tungefanya, maadamu tunamcha Mungu (1 Wakorintho 9:24-27)?*

**15. Je, tunawezaje kuendesha maisha ya kiasi, kulingana na amri za Mungu? Wafilipi 4:13.**

______________________________________________________________________

---

***Uamuzi wangu:*** *Nakusudia kuustawisha mwili wangu kwa njia za kiasili, kulingana na maelekezo ambayo Mungu aliyompatia mwanadamu pale mwanzo.* ❑ *Ndio* ❑ *Hapana*

---

# 28 NAMNA YA KUTATUA MATATIZO YANGU YA KIFEDHA



Kuna watu wengine ambao huongea juu ya bahati njema, lakini Biblia inaeleza juu ya baraka za Mungu. Lakini, je, hali yangu ina nini juu ya mafanikio yangu ya kiuchumi? Hakika. Mfanyabiashara ni lazima awekeze pesa zake vema ili kwamba aje kupata faida. Mkulima ni lazima aoteshe na kutunza vema mazao yake ili aje kupata mavuno mazuri. Iwapo sisi ni wasimamizi, tunapasa kusimamia vema kulingana na uwezo wetu, hususani iwapo mali hizo sio zetu wenyewe. Watu wengi wangetaka kuheshimiwa, na kuhesabu kuwa ni bahati iwapo watatakiwa kuwekeza katika biashara yenye ufanisi mwingi. Hili ndilo hasa ambalo Mungu anatuitia sisi tulifanye. Mungu anatutaka sisi tuwe wabia Wake katika biashara kubwa kabisa ya wote kwa kuusaidia ulimwengu uepuke ile hukumu na kujiandaa kwa ajili ya ufalme Wake wa utukufu ujao. Lakini ni kwa jinsi gani ambavyo naweza kustawi na kutatua matatizo yangu ya kifedha? Nawezaje kubarikiwa na Mungu? Nawezaje mimi kufanya uwekezaji iwapo mimi sijawa mfanya biashara, niotesheje iwapo sijawa mkulima, nizifungeje shughuli za kifedha iwapo mimi sijawa mhasibu ama sijampata mdau awezaye kunisaidia kupata faida niwapo sina mtaji? Mungu anatufunulia sisi juu ya mpango ulio katika Biblia ambao kwa njia yake twaweza kustawi.

## *MMILIKI HALALI WA VITU VYOTE*

**1. Daima mwanadamu hudai kuwa ndiye mmiliki wa mali, hata hivyo, ni nani aliye mmiliki halali wa vitu vyote? Zaburi 24:1, 2; 50:10-12.**

____________________________________________________________

**2. Je, Mungu anasemaje juu ya fedha na dhahabu ambazo mwanadamu anazidai? Hagai 2:8.**

____________________________________________________________

**3. Je, ni neno lipi ambalo tusingelisema iwapo tumeinuka kiuchumi na ni kitu gani tunapasa kukitambua? Kumbukumbu 8:11-14, 17, 18.**

____________________________________________________________

**4. Je, ni juu ya msingi upi ambapo Mungu hudai vitu vyote kuwa ni Vyake?**

a) Kwa sababu Mungu ________________________ (Zaburi 100:3).

b) Kwa sababu tunaokolewa kwa ______________ ya thamani ya Kristo (1 Petro 1:18, 19).

c) Kwani tu _______________________________________________ (Matendo 17:28).

Sio kwamba sisi tumeumbwa tu bali pia tumekombolewa kwa neema ya thamani kubwa. Muda wote tunashikiliwa na ule upendo Wake mkuu. Mambo haya matatu hutufanya sisi kumtambua Yeye kama Mwokozi wetu, Bwana na mmiliki halali wa maisha yetu.

**5. Je, nijiulize nini mwenyewe pale nionapo yale Yesu aliyonitendea na anaendelea kunitendea kila siku? Zaburi 116:12-14.**

____________________________________________________________


## *MAWAKILI WA MALI ZA MUNGU*

**6. Je, tufanyeje na miili, mali, muda na pesa zetu? Je, tumepewa jina gani? 1 Petro 4:10.**


*Kila mmoja kwa kadiri alivyopokea ____________, itumieni kwa kuhudumiana; kama _____________. Kila tulicho nacho ni mali ya Mungu. Sisi ni mawakili tu.*




a) ***Mwili wangu:*** Sisi ni mali ya Mungu (1 Wakorintho 6:19, 20; 10:31). Hebu na tukamtukuze Mungu katika mwili wetu kwa kuitunza katika afya njema. Wala tusiidhoofishe wala kuviharibu vile vyanzo vya nguvu kwa njia ya kula vitu ambavyo huidhuru afya yetu. Hebu na tuutumie mwili wetu na nguvu zake kwa kushiriki katika mpango wa Mungu wa wokovu wa ulimwengu.





b) ***Wakati wangu:*** Mungu anatupatia sisi siku sita ili tufanye kazi na kujitoa kabisa katika zile shughuli zetu wenyewe, bali Mungu anaidai ile siku ya saba, Sabato, kuwa ni Yake, (Kutoka 20:9, 10). Siku hii imewekwa kando na Mungu na kutakaswa; laiti tukiiweka kwenye mambo yetu wenyewe na tusiiadhimishe ipasavyo, hapo tunaiba kutoka kwenye muda ambao ni mali ya Bwana. Hii iliwekwa kwa ajili ya faida yetu sisi wenyewe. Hebu basi na tuutoe muda huu kwa kuongea na wengine juu ya mpango wa ukombozi (Matendo 4:32).




c) ***Vipaji vyangu:*** Je, tunafanyeje na vile vipaji ambavyo Mungu ametupatia sisi? Je, tunavitumia kwa ajili Yake? Kuongea, kuimba, kuwaangalia wagonjwa, kuwafundisha watoto, n.k., hivi vyote ni vipaji ambavyo Mungu ametupatia sisi ili vitumike katika kuutangaza ufalme wa Kristo (Mathayo 28:18-20).

Ule mfano wa talanta ni wa makini na muhimu sana (Mathayo 25:14, 19-30). Tunapasa kufanya kazi kwa kila siku kwa ajili ya Mungu kwa njia ya kuongea na watu wengine juu ya upendo wa Yesu na kufundisha zile kweli ambazo




tunajifunza kutoka katika neno Lake. Tutajiona kuwa na furaha sana pamoja na kuwa vile vipaji vyetu vitakua.

d) ***Pesa zangu:*** Pia tutatakiwa kutoa hesabu kwa Mungu kwa ajili ya pesa tulizodhaminiwa sisi.

*Je, tunaitumia pesa hiyo kwa njia ya ubinafsi, ama je, tupo tayari kusaidia kuhubiriwa kwa ule ujumbe kwa pesa zile ambazo Muumba ametupatia sisi?*

**Je, tunalijibu namna gani lile swali lililo katika Zaburi 116:12: "Nimrudishie Bwana nini Kwa ukarimu wake wote alionitendea?" Tunajibu nini? Mithali 3:9-10.**

______________________________________________________________________

*Hii ndio siri ya mafanikio kiuchimi. Tunapasa kutoa sehemu ya pato letu katika kusaidia kuhubiri ujumbe wa Mungu.*

## *MPANGO WA KIMBINGU*

**7. Je, ni sehemu gani ya mali ambayo Mungu ameidhamini kwetu ambayo anadai kuwa ni Yake? Walawi 27:30-32.**

______________________________________________________________________

*Zaka ni sehemu ya kumi ya pato letu. Kwa ujumla ni kuwa hatumpatii Mungu, maadamu kila kitu ni mali Yake; tunamrudishia sehemu ile na kushikilia sehemu tisa kwa ajili yetu wenyewe. Kwa jinsi hii Mungu huipima imani yetu, uaminifu na upendo kwa ajili ya dunia ambayo inahitaji kupokea nuru ya injili kwa njia ya usaidizi wa kifedha.*

**8. Je, zaka hutumikaje? Hesabu 18:20-24.**

*Badala ya huo* __________________ *watumikiao, maana ni huo utumishi …..*

*Zaka hutumika tu kwa kuhubiri injili, hivyo watumishi wa Mungu wataweza kutenga muda wao kwa ajili ya kuokoa roho. Kwa ajili hii, zaka hukadhiwa kwa mtunza hazina wa kanisa, ambaye hugawa pato hilo na kulipa gharama za matumizi ya watenda kazi.*

**9. Je, zaka ilitumikaje katika Agano Jipya? 1 Wakorintho 9:13, 14.**

*Wale waihubirio injili wanapasa* ______________________________________________

**10. Nyuma kabla ya siku za Musa, Ibrahimu na Yakobo walimtolea Mungu zaka zao. Je, hapa tunafundishwa kutoa kutoka mapato gani? Mwanzo 14:20; 28:20-22.**

______________________________________________________________________

*Zaka, ndoa, na Sabato vilianzia katika paradiso. Mti ule ulikuwa ni wa Mungu nao ndio ule ambao Adamu na Hawa hawakupasa kula kutoka kwake, unaiwakilisha zaka. Nasi hapa tunajaribiwa pia.*

## *KANUNI ZINAZOAMURU UFUKARA NA MAFANIKIO*

**11. Siri kuu ya mafanikio ya kiuchumi ni ipi? Mithali 11:24, 25.**

_______________________________________________________________________________

**12. Je, Biblia inasemaje juu ya matokeo ya ukarimu? 2 Wakorintho 9:6, 7, 10.**

_______________________________________________________________________________

**13. Je, Mungu anawaahidi baraka gani waumini? Malaki 3:10-12.**

*Mungu anasema kwamba wale wanaokishikilia kile kilicho mali Yake Yeye kuwa ni ________________.*

*Mungu anahimiza uaminifu, akisema: "Leteni." Anaturuhusu tumjaribu, kwa vile alivyo mwaminifu juu ya ahadi Zake. "Mjue kama sitawafungulia madirisha ya mbinguni, na kuwamwagieni ___________ __________________." Wale wanaomrudishia Bwana kile kinacholingana Naye wanaweza kueleza juu ya ujuzi wao juu ya jinsi Bwana alivyoishikilia ile ahadi Yake. Ile 90% iliyosalia huenda mbali zaidi ya ile 100% ya wale wasiolipa zaka.*

**14. Je, tutoe nini tena? Malaki 3:8.**

_______________________________________________________________________________

*Sadaka. Hizi zaweza kuwa ni za shukurani, malimbuko (Kumbukumbu 18:4), ya maskini (Wagalatia 2:10; Warumi 15:26). Katika Zaburi 41:1, 2 na Mithali 19:17, hizi ni ahadi kwa wale ambao kwa ukarimu huwapatia maskini.*

## *HITIMISHO*

**15. Je, twawezaje kuwekeza katika benki ya mbinguni? Luka 6:38.**

*Wapeni ____________________________________________ kwa kipimo kile kile mpimacho ______________________________________________________.*

*Mungu awapenda wale watoao kwa moyo wa ukarimu, lakini tunapasa kukumbuka ya kwamba kwa uhalisi hatutoi cho chote, kwa sababu kila kitu ni mali Yake. Pele tunaporejesha kilicho Chake, kwa wepesi tunasema, "Natambua ya kwamba Wewe ndiwe Bwana wangu, nakupenda. Hii ndio faida ya kile ulichonipatia mimi nikisimamie." Naye Bwaba atasema, "Vema, mtumwa mwema na mwaminifu; ulikuwa mwaminifu kwa machache, nitakuweka juu ya mengi; ingia katika furaha ya bwana wako." Mathayo 25:21.*

---

***Uamuzi wangu:*** *Ninataka kuwa mtumwa mwaminifu wa Mungu na kushiriki katika kazi Yake.*
❑ *Ndio* ❑ *Hapana*

---

# 29 UZURI HALISI



Uzuri halisi una nini ndani yake? Twawezaje kuupata?

Kulikuwako na dada fulani mwenye kuvutia sana, uso wake ulikuwa mzuri sana, mwili wake ulikuwa mwembamba na wenye ulinganifu. Alikuwa na nywele nzuri za hariri, na ngozi laini ya waridi. Angeweza kushinda katika shindano la warembo. Kijana fulani wa kiume aliyepata kumpenda sana akapata nafasi ya kumfahamu katika mazingira yake halisi. Mara akatambua ya kwamba alikuwa ni mchoyo, mwenye kiburi na mwongo na kujionesha katika kutokuwa na nidhamu. Kijana yule akakatishwa tamaa sana, kwa sababu alikuwa amedanganywa tu na ule mwonekano wake.

Uzuri halisi haupatikani katika mwonekano wa nje ama jinsi ile mtu anavyojiweka, kama vile kuwa na "make up", kuvalia vito vya thamani ama mavazi yenye darizi, bali ni katika tabia ya kiungwana na kuvutia.

Inapendezaje kwa kuwa pamoja na mtu aliye na tabia nzuri hata kama hana uzuri wa kimaumbile!

Sio jambo la muhimu sana jinsi vile watu wanavyotuona; jambo tunalolitafuta ni vile Mungu atuonavyo sisi.

## *PAMBO LA NAFSI*

1. **Je, uzuri halisi unaitwaje, ule unaong'aa nje tokea ndani, kwa msaada wa Roho Mtakatifu? 1 Wathesalonike 4:3, 7; Warumi 6:22.**

   ________________________________________________________

   *Pale mfinyanzi anaposhughulika na udongo na kutengeneza chungu, hufanya hivyo nje tokea ndani. Mungu pia anataka kutubadilisha sisi ndani, hivyo vielelezo vya utakatifu Wake vyaweza kuonekana kwa nje.* ***Hatua hii huitwa utakaso.***

2. **Je, ni sehemu ipi ya ubinadamu wetu inayotakaswa kwa njia ya utendaji wa Roho Mtakatifu ndani yetu? 1 Wathesalonike 5:23.**

   ________________________________________________________

   *Mawazo yetu, hisia na matendo yetu ni lazima vitakaswe. Katika namna yetu ya ulaji, uvaaji, uongeaji na kuishi, yapasa vitambulishe ya kwamba sisi tu wafuasi wa Yesu.*

3. **Je, ni ushauri gani unaotolewa kuhusu uvaaji wetu pamoja na mwonekano wetu? 1 Timotheo 2:9, 10.**

   ________________________________________________________

4. **Je, mapambo halisi ya mwanamke Mkristo yana nini? 1 Petro 3:2-5.**

   ________________________________________________________

5. **Je, ni kitu gani hasa kinachoongeza mwonekano wa mtu? Mithali 15:13.**

   ________________________________________________________

   *Wanawake wa Isaraeli wa kale waliagizwa na Mungu kujivika utaji wa samawi ulioshonelewa katika pindo za mavazi yao ili kuwabainisha wao kutokana na wale wa mataifa. Je, upindo huu wa samawi unaotutenga sisi kando ni nini? Staha katika namna ya uvaaji wetu, tukijiepusha na mapambo ya vito vya thamani, kufanya "make-up" na kutia rangi katika nywele, mambo ambayo hudhuru afya yetu na kuongeza ubatili na kumharibu mtu yule aliyeumbwa na Mungu. Kwa kufuata matendo kama hayo,*

*tunamwambia Muumba, "Mimi sina furaha kutokana na jinsi ulivyoniumba." Uso wenye furaha, katika hali yake ya asili, na tabia ya upole, hivi na viwe ndio mapambo halisi ya Mkristo.*

**6. Je, ni aina gani ya mavazi ambayo hayampendezi Bwana? Kumbukumbu 22:5.**

__________________________________________________________________

**7. Je, Biblia imesema cho chote juu ya urefu wa nywele za mwanamke? 1 Wakorintho 11:14, 15.**

__________________________________________________________________

- Je, Mungu atapendezwa na mtu mchafu, timutimu? Aghalabu, hapana. Tunapasa kuvaa vitu vilivyo katika mwonjo mzuri, tununue ama kushona nguo zenye ubora, pale inapowezekana, na kujawa na kanuni za kuhifadhi afya.
- Tupasa kueneza upya, uungwana, pamoja na kutokuwa na madoido ili kwamba kila mmoja aweze kuona kitu fulani cha tofauti kwetu. Hata hivyo, tunapasa kuepuka kuvutiwa na mitindo na maoni ya watu wengine.
- Hebu na tudumishe tabia njema ya pekee, tukijaribu kuishi kwa ajili ya Mungu. Furaha ya kumpenda na kumtii Yesu itakuwa ndio ijara yetu. Katika Isaya 3:16-26, twaweza kusoma juu ya ajali ya majisifu na kutotii.

## *BURUDANI*

**8. Je, ni kanuni ipi katika Biblia tuwezayo kuitumia kwa burudabi na starehe? Wafilipi 4:8.**

__________________________________________________________________

*Kulingana na nuru ya aya hii, na tufikie kwenye kuchukua chaguo jema la burudiko. Angalia yale unayoyasoma, programu za Luninga yako, michezo, n.k.*

**9. Je, maisha yetu ya kiroho yaweza kuathirika na utazamaji wa mambo haya ya fujo, maasi na uasherati, hata kama sio vitendo halisi? Isaya 33:15-17.**

__________________________________________________________________

**10. Je, ni ushauri gani unaotolewa kwa mtu yule anayependa kuangalia mambo mazuri yenye kumwinua? 1 Yohana 2:15-17.**

__________________________________________________________________

**11. Je, Mungu anawaelekeza nini wale wanaotaka kuonesha shukurani kwa Yesu kwa namna ambavyo amewaokoa? 1 Petro 1:13-19 (taja mambo 3).**

__________________________________________________________________

*Kuna wale ambao wanafikiri ya kwamba wanaweza kuinunua mbingu kwa njia ya matendo yao, lakini hili haliwezekani.*

**12. Je, ni nani pekee atuhamasishe sisi kumtii Mungu? 1 Petro 2:21-25.**

__________________________________________________________________

*Pale Sauli alipokuwa mtesaji Naye Yesu alipomtokea na kumtaka amfuate, aliuliza, "Je, Bwana wataka nitende nini (Matendo 9:6)?" Huu unapasa kuwa ndio msimamo wetu.*

*Tutapokea jibu iwapo tutajiuliza wenyewe: "Je, Yesu angefanya nini kwa niaba yangu?" Hebu na tumwambie: Bwana, nataka kufanya vile ambavyo ungependa kufanya laiti ukiwa mahali pangu," Naye atatuonesha yale tupasayo kutenda.*

## *HITIMISHO*

**13. Je, ni wapi tuwezapo kupata nguvu ya kubadilisha tabia na desturi zetu? Wafilipi 2:13; 4:13.**

____________________________________________________________

**14. Je, ni ujira gani unawasubiri wale washindi? Marko 10:28-30; 1 Wakorintho 9:23-27.**

____________________________________________________________

***Uamuzi wangu:*** *Nataka kumtukuza Mungu kwa njia ya uvaaji wangu na kuielekeza mwenyewe kwa kulingana na mapenzi Yake.* ❑ *Ndio* ❑ *Hapana*

# 30 SIRI YA MAFANIKIO




Kila mwanadamu anataka kuwa mwenye mafanikio.

Vijana wanataka kufanikiwa katika masomo yao; mama anataka mafanikio katika elimu ya watoto wake, mwanamme ama mwanamke anataka mafanikio katika maisha ya fani yake; mwanasiasa anataka mafanikio katika shauku yake ya kupata madaraka; mwanariadha anataka mafanikio ya kuwa mshindi; mtu mgonjwa anataka mafanikio katika juhudi zake za kurejesha afya. Mkristo pia anataka mafanikio katika kutambuliwa pamoja na Kristo na kuurithi uzima wa milele. Je, twawezaje kufanikisha hili? Je, ni kipengee gani ambacho Biblia inakitoa ili kutusaidia sisi kufaulu katika maisha haya ya kawaida na yale ya kiroho? Mungu anataka mafanikio yetu na kuwa na afya njema (3 Yohana 2), Naye anataka kutupatia sisi nguvu ya kuwa na mafanikio makubwa.

## *SIRI KUMI NA MBILI KWENYE MAFANIKIO*

1. **Utoe moyo wako kwa Yesu na kuupokea wokovu na kuhesabiwa haki Yake (Warumi 5:1). Je, ni maneno gani anayokuambia wewe? Mithali 23:26.**

   ______________________________

2. **Mweke Mungu katika nafasi ya kwanza. Je, maneno ya Yesu juu ya jambo hili yalisemaje? Mathayo 6:33.** ______________________________

3. **Tunapasa kuukiri udhaifu wetu wa kibinadamu na kuunganisha moyo wetu na ule wa Kristo, tukitumainia ile neema Yake kwa kila siku. Je, muunganiko huu unalinganishwa na nini? Yohana 15:4, 5.**

   ______________________________

4. **Kila siku unapasa kulichunguza neno la Mungu kwa makini (Matendo 17:11). Je, kusudi letu na liwe ni lipi? Kumbukumbu 17:19.**

   ______________________________

5. **Daima na uombe. Je, Danieli aliomba mara ngapi kwa siku? Danieli 6:10.**

   ______________________________

6. **Uwe na imani. Twaweza kufanya nini pasipo na imani? Waebrania 11:6.**

   ______________________________

7. **Hudhuria mikutano ya kikanisa (Waebrania 10:25). Je, desturi ya Yesu ilikuwaje? Luka 4:16.**

   ______________________________

8. **Samehe na kupenda. Je, ni mfano gani ambao daima ungetuhamasisha sisi? Wakolosai 3:13, 14.**

   ______________________________

9. **Ufuate mfano wa Yesu katika utii juu ya amri Zake. Je, ule wokovu umeahidiwa kwa nani? Waebrania 5:8, 9.**

   ______________________________

**10. Ukawe nuru kwa wengine. Je, Bwana anataka sisi tuwe nini? Matendo 13:47.**

______________________________________________________________________

*Kwa njia ya kazi na mali zetu, tunapasa kushiriki katika wokovu wa wengine.*

**11. Uwe jasiri. Je, ni ahadi gani ambayo tungeishikilia? Waebrania 10:23.**

______________________________________________________________________

*Katika nyakati za majaribu, hebu daima na tukumbuke ya kwamba Mungu haturuhusu sisi tujaribiwe kuliko tunavyoweza kustahimili (1 Wakorintho 10:13).*

**12. Tumtumaini na kumruhusu Mungu afanye kazi ndani yetu. Je, ni ahadi gani ambayo Bwana anawapatia wale wanaojitoa kikamilifu kwa Yesu? Wafilipi 2:12, 13.**

*Kwani ni Mungu* ______________________________________________________

*Iwapo tumejitoa kwa Yesu kwa kujiweka wenyewe upande mnyofu, Mungu ataweka ndani ya mioyo yetu ile shauku ya kumtii Yeye na atatupatia sisi ile nguvu muhimu ili kufanya hivyo. Anaivuta nia yetu kwa Roho Wake Mtakatifu. Ametuita sisi na anataka kutufanya sisi tuwe wenye fiuraha.*

## *JE, MAFANIKIO HUTOKANA NA BAHATI?*

**13. Je, ni fursa gani ambayo Mungu humpatia kila mwanadamu? Kumbukumbu 30:14-16, 19.**

______________________________________________________________________

*Mungu anataka sisi tuokolewe, lakini wala hatatulazimisha. Ametupatia hiari, Naye ameweka mbele yetu njia mbili: uzima ama mauti, laana ama baraka. Tunapokea uzima na baraka iwapo tunatii amri Zake. Jinsi anavyotuita kwa upole! Chagua uzima ili kwamba wewe na wazao wako mpate kuishi. Alifanya kila kitu ili kutuokoa na kutupatia ushindi. Hivyo, inategemea juu yetu sisi kufanya chaguo sahihi.*

**14. Je, ni ushauri gani ambao Yesu hutupatia sisi? Yohana 12:35, 36.**

______________________________________________________________________

- Kufanikiwa na kushindwa kwetu maishani-wokovu ama maangamizi-viko mikononi mwetu wenyewe. Ujumbe wa Eliya unakuja kwetu, “Mtasita-sita katikati ya mawazo mawili hata lini? Bwana akiwa ndiye Mungu, mfuateni; bali ikiwa Baali ni Mungu, haya! Mfuateni yeye. (1 Wafalme 18:21).”
- Tayari umeupokea wito wa Yesu. Kwa jinsi hii, umepata kuziona zile kweli bora kabisa walizopata kupewa wanadamu. Je, witikio wako utakuwaje?
- Yesu alionesha upendo Wake mkubwa katika kile kipindi cha utumishi Wake hapa dunuiani; aliteseka hata Gethsemane na pale Kalvari. Hebu basi kafara Yake isiwe bure!
- Aliteseka kwa maumivu yasiyosemekana, alipigwa mijeredi, alidhihakiwa na umati uliomkasirikia, dharau kali za wale aliopata kuwasaidia, na kusalitiwa naye yule aliyepata kutembea pamoja Naye. Aliubeba ule mzigo mzito wa msalaba, majeraha ya ile miiba yanayotoa damu kichwani Mwake, pamoja na maumivu yasiyobebeka ya ile misumari ikiupenya mwili Wake pale msalaba ulipoinuliwa. Zaidi ya yote haya, alizibeba dhambi za ulimwengu huu usio na uaminifu katika ule mwili ulioparuliwa na kudharauliwa, uliochoka mno kabisa.
- Hata hivyo, aliwasamehe wauaji Wake pamoja na wale waliomsulibisha pamoja na dhambi na makosa yao. Je, tutaiacha kafara hii bure?
- Yeye alifanya kila jambo kwa ajili ya kutuokoa sisi, na hivi leo analitaka jibu kutoka kwetu. Hebu na likawe ni jibu la kukubali! Anatupatia sisi nafasi mbinguni pamoja na uzima wa milele na anataka tu moyo wetu. Je, hutampatia?

## *AHADI SABA ZA PEKEE ZA MUNGU*

**Kwake yeye ashindaye…**

1. "Nitampa kula matunda ya mti wa uzima (Ufunuo 2:7)"
2. "Hatapatikana na madhara ya mauti ya pili. (Ufunuo 2:11)".
3. "Yeye ashindaye nitampa baadhi ya ile mana iliyofichwa, nami nitampa jiwe jeupe, na juu ya jiwe hilo limeandikwa jina jipya (Ufunuo 2:17)."
4. "Nitampa mamlaka juu ya mataifa (Ufunuo 2:26)."
5. "Atavikwa hivyo mavazi meupe, wala sitalifuta kamwe jina lake katika kitabu cha uzima (Ufunuo 3:5)."
6. "Nitamfanya kuwa nguzo katika hekalu la Mungu wangu, wala hatatoka humo tena kabisa (Ufunuo 3:12)."
7. "Nitampa kuketi pamoja nami katika kiti changu cha enzi (Ufunuo 3:21)."

---

***Uamuzi wangu:*** *Ninataka nihesabiwe miongoni mwa wale washindi na kuishi maisha ya ushindi pamoja na Yesu.* ❑ *Ndio* ❑ *Hapana*

---

# Somo la 20-30

## MASWALI YA TAFAKARI

Kusudi la orodha hii ya maswali yanayohitaji majibu yake ni kutathmini uelewa wako juu ya yale yaliyomo katika masomo haya ambayo tayari umeyamaliza. Iwapo unapenda, unaweza kuyakamilisha mbele ya mkufunzi huyu na kisha uyaweke pamoja maswali yale uliyoyajibu kwa usahihi. Iwapo una swali lo lote, uyapitie upya masomo haya ama umwulize mkufunzi wako.

**1) Orodhesha maana ya mifano ya wanyama ambao Danieli aliwaona katika maono.**

a. Simba mwenye mabawa ____________________________

b. Dubu ____________________________

c. Chui mwenye mabawa ____________________________

d. Mnyama wa kutisha ____________________________

**2) Je, ile pembe ndogo ingefanya nini kwa wale waumini wa kweli?**

________________________________________________________________________________

**3) Je, ni majuma mangapi ya kinabii yaliyoamriwa juu ya watu wale Wayahudi?**

________________________________________________________________________________

**4) Je, zile siku 2,300 zinaishia katika mwaka gani?**

________________________________________________________________________________

**5) Je, ni nini kingeanza kule mbinguni mnamo 1844, kulingana na unabii wa Danieli 8:14?**

________________________________________________________________________________

**6) Je, kazi ya Kristo kule mbinguni ni ipi?**

________________________________________________________________________________

**7) Je, ni kielelezo gani kimetumika katika kitabu cha Ufunuo kuliwakilisha kanisa?**

________________________________________________________________________________

**8) Je, ni tabia gani mbili za wale wanaoliunda kanisa la Bwana?**

________________________________________________________________________________

**9) Mnyama yule anayetokea kutoka baharini, mwenye vichwa 7 na pembe 10 anawakilisha:**

a. Mamlaka ya Kisiasa b. Mamlaka ya Kipapa c. Wanaoamini kuwa hakuna Mungu

**10) Mnyama yule anayetokea katika nchi, mwenye pembe 2 anawakilisha:**

a. Urusi b. China c. Marekani

**11) Je, masharti ya kuingia katika ufalme wa Mungu ni yapi?**

a. Kwenda kanisani b. Kutenda mambo mema c. Kuzaliwa upya

12) Je, mtu unawezaje kumtofautisha nabii wa kweli na yule wa uongo? (taja mambo 2)

a. ____________________________________________

b. ____________________________________________

13) Je, mwanamke aweza kuwa nabii?

____________________________________________

14) Je, ni chakula gani kilicholiwa pale Edeni?

____________________________________________

15) Orodhesha funguo 2 kwenye maisha ya kiafya.

a. ________________________________

b. ________________________________

16) Je, ni asilimia ngapi ya pato letu inapasa kutengwa kwa ajili ya utumishi wa Mungu?

____________________________________________

17) Je, siri ya mafanikio ni ipi?

____________________________________________

18) Je, ni pambo gani ambalo Mkristo angejitahidi kuwa nalo?

____________________________________________

19) Je, ni kanuni gani ambayo imeoneshwa katika maburudisho na yale yanayopendelewa na Wakristo?

____________________________________________

20) Taja siri mojawapo ya ushindi kwenye maisha ya Kikristo.

____________________________________________



# KUZITAFAKARI SEMI

Semi kadha zimeandaliwa, ambazo hutumika kama kwa kuchunguza nazo huwa zinafanya maamuzi yetu makuu.

Orodha hii yaweza kuwa yenye manufaa sana katika maendeleo yetu ya maisha haya ya Kikristo.

1. Ninaamini ya kwamba Biblia yote ni neno la Mungu lililovuviwa.
2. Ninaamini ya kwamba tunaishi katika siku za mwisho za historia ya dunia hii na kwamba Yesu Kristo atarudi haraka katika nafsi na namna ya kuonekana.
3. Kando ya Kristo hakuna njia nyingine ya wokovu.
4. Mimi nahesabiwa haki kwa imani pekee, nayo matendo ni matunda tu ya imani na uthibitisho wa upendo wangu.
5. Ninaamini ya kwamba utakaso ni kazi ya Kristo ndani yangu, kwa kupitia kwa Roho Mtakatifu.
6. Kila siku ninasali kwa Bwana, pia ninaombea baraka juu ya milo yangu.
7. Ninaamini juu ya uthabiti wa zile Amri Kumi.
8. Ninaami ya kwamba Sabato ndio siku sahihi ya kupumzika nami nataka kuiadhimisha.
9. Wafu hawajui lo lote nao wamelala usingizi hata ule ufufuo wa mwisho.
10. Ninaamini ya kwamba ninapasa kutafuta msaada kutoka kwa Yesu pekee, na wala sio kutoka kwa waonaji, waponyaji, wanajimu ama watu wa mizimu.
11. Ninaamini juu ya uzima wa milele na ya kwamba Mungu ataumba nchi mpya baada ya ile miaka elfu moja.
12. Mnamo 1844, hukumu ya upelelezi ndipo ilianza na Yesu akiwa katika Mahali Patakatifu Mno pa hekalu la mbinguni.
13. Kanisa la kweli la Mungu linafahamika kwa kuzishika amri za Mungu na kuwa na imani ya Yesu.
14. Nataka kubatizwa ili kwamba niwe sehemu ya mwili wa Kristo, ambao ni kanisa Lake.

15. Ninaamini ya kwamba Mungu amejifunua Mwenyewe kwa njia ya roho ya unabii katika Ellen G. White.

16. Napenda kujipendezesha mwenyewe kwa njia asilia, kulingana na miongozo ambayo Mungu aliwapatia wanadamu pale mwanzo.

17. Ninakiri ya kwamba vyote nilivyo navyo ni mali ya Mungu. Napenda kumpanga kama mshirika wangu kwa kutoa zaka na sadaka zangu kwa shukurani Kwake.

18. Nakusudia kuvaa kwa kulingana na kawaida za Mkristo na kujifurahisha mwenyewe kwa kulingana na mapenzi ya Mungu.

19. Napenda kuwashirikisha na wengine lile neno la Mungu na kuwaeleza juu ya wokovu.

20. Napenda kuhesabiwa miongoni mwa washindi na kuishi maisha ya ushindi pamoja na Kristo.

**Mahali na namba ya simu ya kanisa lililo karibu zaidi**

# Anwani za Mawasiliano

## NORTH AND CENTRAL AMERICA

**Belize**: Email: info@labibliatienerazon.org
**Canada**: www.4truth.ca / Email: mail@4truth.ca
**Jamaica**: Tel.: (+1) 876-489 1658
imssdajamaica@gmail.com
**Puerto Rico**: Tel./Fax: (+1) 787-726-6192
Email: info@labibliatienerazon.org
**USA**: Email: info@sda1888.org
Web: www.sda1888.org
**Other Caribbean Islands**:
info@labibliatienerazon.org

## EUROPE

**Germany:** Tel.: (+49) 5406-8989952
geschaeftsstelle@reform-adventisten.net
**Italy:** Tel.: (+390) 861-781 110
missionicristiane@virgilio.it
**Spain:** Tel.: (+34) 96-151 2844
info@asdimores.org/asdimores@gmail.com
**The Netherlands:** Tel.: (+31) 313-416 222
Rehoboth@ZDAreformatie.org
**United Kingdom:** Tel.: (+44) 7766322052
treasury.bf@hotmail.com

## AFRICA

**Botswana:** imstso1844@gmail.com
**Cameroon:** Cel. & WhatsApp: (+237) 6 5315 6974
imscameroon1994@gmail.com
**Gambia:** imsgambia1914@gmail.com
**Kenya:** Cel.: (+254) 727-928-488
imskenyaunion@gmail.com
**Lesotho:** AfricanDivision@sda1844.org
**Liberia:** Tel.: (+231) 6-530 668
imssdarmlib2009@yahoo.com
**Malawi:** Cel.: (+265) 884 514 363
malawiunion@hotmail.com
**Nigeria:** Tel.: (+234) 803-744-7190
imsnigeriafield@gmail.com
**Rwanda:** Cel.: (+250) 788 660 278
rwanda_field@yahoo.com
**Seychelles:** imsseychelles1888@gmail.com
**Sierra Leone:** inter.miss.sl@gmail.com
**Sudan:** imssdarmssudanfield@yahoo.com
**South Africa:** Tel.: (+27) 76-615-9434
imssouthafricaunion@gmail.com
**Tanzania:** Tel.: (+255) 565 533 298
unoftzimssdarm@yahoo.com
**Uganda:** Cel.: (+256) 772 370 673
uimssda1844@yahoo.com
**Zambia:** Tel.: (+260) 211-282-805
zamunion@gmail.com
**Zimbabwe:** Cel.: (+263) 712 775 775
imssdazimfd@yahoo.com

## ASIA

**Bangladesh:** bangladeshadventistrms@gmail.com
**China:** Tel. & Fax: (+86) 24-2471 8125
ims1888@163.com
**India:** Cel.: (+91) 98-6203-0096
crosswell.rimsu@gmail.com
imsindia@rocketmail.com
**Indonesia:** Tel. & Fax: (+62) 21-860 7244
imssdarmjkt@gmail.com
annabelllgm@gmail.com
**Malaysia:** AsianDivision@sda1844.org
**Myanmar:** AsianDivision@sda1844.org
**Pakistán:** AsianDivision@sda1844.org
**Philippines:** Tel.: (+63) 32-269-1004
AsianDivision@sda1844.org
**South Korea:** Tel.: (+82) 2-220 1233
AsianDivision@sda1844.org
**Sri Lanka:** Tel.: (+94) 777-566 591
AsianDivision@sda1844.org

## PACIFIC

**American Samoa:** Tel.: (+684) 252 1870
sefoims_amsamoa@yahoo.com
**Australia:** Tel.: (+61) 2-9896 0150
OceaniaDivision@sda1844.org
**Cook Islands:** OceaniaDivision@sda1844.org
**Fiji:** Tel.: (+679) 3548477 / Cel.: (+679) 9533988
sanailaravia@yahoo.com
**New Zealand:** Tel.:0 (+64) 3-352 5023
OceaniaDivision@sda1844.org
**Papua New Guinea:** Cel.: (+675) 721 70 825
OceaniaDivision@sda1844.org
**Samoa:** Cel.: (+685) 7208011 / Cel.: (+685) 7249047
OceaniaDivision@sda1844.org

**INTERNATIONAL MISSIONARY SOCIETY**
**SEVENTH-DAY ADVENTIST CHURCH REFORM MOVEMENT**
**General Conference**

625 West Avenue • Cedartown, GA 30125 • U.S.A.
P.O. Box S • Cedartown, GA 30125 • U.S.A.
Telephone (+1) 770-748-0077 • FAX (+1) 770-748-0095
E-mail info@sda1844.org

---

**INTERNATIONAL MISSIONARY SOCIETY**
**SEVENTH-DAY ADVENTIST CHURCH REFORM MOVEMENT**
**TANZANIAN UNION**

P.O. Box 70908
Email: unoftzimssdarm@yahoo.com
Dar es Salaam Tanzania

biblewell.org

**www.asd1844.org**